**BREAKING NEWS**
SUPA JACKPOT
1,008,534,842/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 4

**SERIKALI** yatoa msimamo kodi kwa TIN, kikokotoo cha mafao na mikopo ya halmashauri




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Juni 25, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580987

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


### HUKU ADA IKIFUTWA:

# Hivi ndivyo ilivyo michango shuleni

UKURASA 2

1. Gharama za ulinzi wa shule
2. Kukodi godoro kwa mwaka
3. Malipo ya mpishi wa shule
4. Ukarabati samani, matibabu
5. Fedha za tahadhari, taaluma
6. Wanafunzi wajinunulia vitabu



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda

# Askari polisi apigwa risasi kifuani akijihami

UKURASA 3

## Meli kubwa yatia nanga na shehena ya mbolea

UKURASA 4

**MICHEZO** YANGA SHANGWE MBEYA, SIMBA IKIMNASA MPOLE UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akisalimiana na Rais wa Rwanda, Paul Kagame, walipokutana katika ufunguzi wa Mkutano wa Wakuu wa Serikali wa Nchi Wanachama wa Jumuiya za Madola (CHOGM 2022), jijini Kigali, nchini Rwanda jana. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola, Patricia Scotland. **PICHA: OMR**

## Kina Mdee kortini tena, wafungua kesi yao upya

**Na Grace Gurisha**

WABUNGE 19 wa viti maalumu waliofutwa uanachama wa CHADEMA, wamewasilisha tena maombi namba 27/2022 ya kuomba kibali cha kufungua kesi ya kupinga kuvuliwa uanachama katika Mahakama Kuu Masjala Kuu, Dar es Salaam.

Vilevile, wabunge hao wamewasilisha maombi madogo namba 16/2022 ya kuiomba mahakama kutoa zuio la muda kutochukuliwa hatua yoyote ikiwamo wabunge hao kubaki na hadhi yao hadi kesi ya msingi itakaposikilizwa na kutolewa uamuzi.

Maombi hayo yaliwasilishwa mahakamani huko juzi na mawakili wao; Ipilinga Panya, Aliko Mwamanenge na Egnus Kiratu, baada ya kufanya mabadiliko ambayo yalisababisha maombi yao kutupwa na Jaji John Mgeta.

Wakili Panya alidai kuwa siku uamuzi ulipotolewa na Jaji Mgeta, Juni 22 mwaka huu, wa kutupa mapingamizi, walirudi ofisini mara moja na kuanza kuyafanyia kazi na ndani ya saa tatu walimaliza kurekebisha kasoro hizo za kisheria.

Alidai kuwa Juni 23 walifanikiwa kufungua maombi yao saa mbili asubuhi kwa njia ya mtandao na kupata namba hizo, wakiwashauri wabunge hao wamwandikie Spika wa Bunge barua ya kumweleza kwamba tayari wameshafungua maombi mengine mahakamani.

Pia alidai wamewashauri wabunge hao kwamba wasizingatie mambo ambayo yanaendelea katika mitandao ya kijamii kwamba hakuna kesi tena, kwa kuwa wao ni mawakili na wanajua wanachokifanya.

"Nilisafiri usiku kucha kwenda Dodoma kwa ajili ya kuwasainisha waleta maombi, ambapo niliweza kufanikisha suala hilo, nikarudi Dar es Salaam na kuendelea na taratibu zingine za kufaili maombi hayo na tulifanikiwa," alidai Panya.

Jaji Mgeta alikubaliana na baadhi ya mapingamizi kati ya saba yaliyowasilishwa na Wakili wa Chadema, Peter Kibala, huku mengine akibainisha dosari ambazo zinaweza kurekebishwa na mengine kuyatupilia mbali.

# Hivi ndivyo ilivyo michango shuleni

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI serikali ikipendekeza kufuta ada kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita, imebainika kuwapo michango mingi shuleni ambayo katika baadhi ya shule inazidi hata ada inayopendekezwa kufutwa.

Serikali kupitia kwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, iliwasilisha bungeni mapendekezo hayo ya kufuta ada hiyo Juni 14 mwaka huu. Jana Bunge liliridhia mapendekezo hayo lilipopitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

Akichangia hoja ya mapendekezo ya bajeti hiyo jana bungeni, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema Sh. 70,000 kwa ajili ya ada ya kidato cha tano na sita kilichofutwa ni kikubwa kwa familia.

Alisema wanaodhani ni kiasi kidogo watambue kuwa kuna wazazi walishindwa kutoa kiasi hicho kusomesha watoto wao, hivyo inakwenda kupunguza mzigo, huku akiahidi kufuatilia kero ya michango mingi shuleni.

"Ni sehemu ya gharama ya kusoma, tutapitia mingozo yote kwa kushirikiana na Hazina na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili kusiwe na mzigo mkubwa unaokinzana na azma ya kutoa elimu bure, na kwamba watapitia taratibu zote za kujiunga ili kujiridhisha,"alifafanua.

Alisema lengo ni kupunguza michango ambayo haina maana na tija kwa wananchi inayokwaza azma ya elimu bure.

"Wazazi wanapitia mengi, wakiona mtoto amefaulu, wanaona ni mzigo. Kuna mambo ya sare, ninashukuru Wizara ya Fedha na Mipango kwa kutenga fedha kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambayo inaainisha familia zinazohitaji msaada na itapunguza mzigo kwa familia," alisema.

**MICHANGO SHULENI**

Katika ufuatiliaji wake, Nipashe imebaini kuwa, mwanafunzi anayejiunga kidato cha tano mwaka huu katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Ashira iliyoko Moshi Vijijini mkoani Kilimanjaro, anatakiwa kulipa jumla ya Sh. 175,000 kwa mwaka, ziikiwa ni ada ya shule Sh. 70,000, ukarabati wa thamani Sh.15,000, kukodi godoro Sh.10,000, kitambuliho Sh. 5,000, taaluma Sh. 20,000, wapishi Sh. 20,000, huduma ya matibabu binafsi Sh. 10,000, ulinzi Sh. 20,000 na tahadhari Sh. 5000.

Vilevile, anatakiwa kwenda na vifaa kwa ajili ya matumizi ya shule ikiwamo ufagio wa ndani, mopa, jembe, panga na ufagio wa chelewa, jembe, rato, ndoo ya plastiki, panga, brashi ya kusafishia ndoo na fyekeo pamoja na vitabu, mahitaji hayo yakigawanywa kulingana na tahasusi wanazosoma.

Kwa mwanafunzi anayejiunga na Shule ya Eekondari Juhudi iliyoko jijini Dar es Salaam, anatakiwa kulipa jumla ya Sh. 128,000, zikijumuisba ada ya shule, tahadhari Sh. 5,000, ulinzi Sh. 5,000, dawati /ukarabati wa samani Sh. 15,000, nembo ya shule Sh. 3,000, kitambulisho na picha Sh. 5,000, mazingira Sh. 10,000, afya Sh. 5,000, umeme Sh. 10,000, karatasi Sh. 10,000 na mtihani wa moko Sh. 20,000.

Kwa Shule ya Sekondari Ntiko iliyoko mkoani Singida, mahitaji yake kwa mwanafunzi anayejiunga nayo kidato cha tano mwaka huu ni: Ada ya shule Sh. 70,000, Sh. 15,000 kwa ajili madawati, Sh. 20,000 kwa ajili ya taaluma, Sh. 5,000 ya tahadhari, Sh. 30,000 ulinzi na wapishi, Sh. 20,000 mitihani ya kujipima Sh. 6,000 kitambulisho, Sh. 10,000 huduma ya kwanza na matibabu na Sh. 12,000 ya ukarabati.

Mwanafunzi huyo pia atatakiwa kwenda na vifaa kwa ajili ya matumizi ya shule ikiwamo ufagio wa ndani, mopa, jembe, panga na ufagio wa chelewa.

Katika Shule ya Sekondari Lindi, mahitaji ya lazima Sh. 108,000 ambayo mzazi anatakiwa kulipa kupitia benki.

Michango hiyo ni taaluma Sh. 20,000, ukarabati Sh. 15,000, huduma ya afya Sh. 10,000, malipo kwa vibarua, wapishi, walinzi Sh. 30,000, kitambulisho Sh. 6,000, nembo Sh. 2,000, mtihani wa utamilifu, Sh. 20,000, tahadhari Sh. 5,000 pamoja na fulana mbili zinazopatikana shule kwa Sh. 15,000.

Katika Shule ya Sekondari ya Ufundi Mtwara, michango inayotakiwa kulipwa ni Sh. 116,000 ambayo inahusisha ukarabati wa samani Sh. 15,000, kitambulisho na picha Sh. 6,000 na taaluma Sh. 20,000.

Mingine ni wapishi, walinzi na vibarua Sh. 30,000, nembo ya shule Sh. 2,000, huduma ya kwanza Sh. 10,000, kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya CHF Sh. 5,000, mitihani ya kujipimia Mock Sh. 20,000, tahadhari Sh. 5,000 na michezo Sh. 3,000 pamoja na ada Sh. 70,000, ambayo serikali imependekeza ifutwe.

Shule ya Sekondari Soya iliyopo Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma, fomu ya kujiunga inaonyesha kuwa kila mwanafunzi anapaswa kulipa tahadhari Sh. 5,000, mpishi na kuni Sh. 20,000 kwa mwaka, huduma ya maji Sh. 15,000 kwa mwaka, huduma ya umeme Sh. 10,000 kwa mwaka na kuboresha taaluma Sh. 20,000 kwa mwaka.

Mingine ni mchango wa mlinzi Sh. 10,000 kwa mwaka, ukarabati wa samani Sh.10,000 kwa mwaka, mchango wa mahafali Sh. 10,000, Mchango wa kununua kemikali Sh. 10,000 kwa mwaka, mchango wa UMISETA Sh. 5,000 kwa mwaka, Ada Sh. 70,000 kwa mwaka au Sh. 35,000 kwa muhula.

Kwa Shule ya Sekondari Njombe, mwanafunzi anatakiwa kulipa ada ya Sh. 70,000, ukarabati Sh. 15,000, kitambulisho Sh. 6,000, taaluma Sh. 20,000, kuwalipa watumishi kama walinzi na wapishi Sh. 30,000, nembo Sh. 2,000, tahadhari Sh. 5,000, mahafali 10,000, mitihani endelezi 20,000, hivyo kufanya jumla ya michango yote kuwa Sh. 188,000.

Michango katika Shule ya Sekondari Tukuyu ni ada Sh. 70,000, ukarabati Sh. 15,000, kitambulisho Sh. 6,000, nembo Sh. 2,000, taaluma Sh. 20,000, wapishi na vibarua wengine Sh. 30,000, matibabu Sh. 10,000, tahadhari Sh. 5,000 na mitihani ya kujipima Sh. 20,000, hivyo jumla ya michango yote ni Sh. 178,000.

Michango ya aina hiyo pia imeshuhudiwa na Nipashe katika shule zingine nyingi za kidato cha tano na sita, zikiwamo: Kate (Rukwa), Kafule (Songwe), Songe (Mara) na Shule ya Sekondari ya Wasichana Iringa.

# HABARI KITAIFA




Sehemu ya shehena ya viuatilifu aina ya salfa, ikishushwa kutoka kwenye meli kubwa iliyotia nanga katika Bandari ya Mtwara jana, ikitokea Saudi Arabia. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# Kikokotoo kipya mafao wastaafu kuanza Ijumaa

**Na Salome Kitomari,**

DODOMA

SERIKALI imefafanua kuhusu fomula mpya ya kikokotoo cha mafao kuwa kitaanza kutumika Julai Mosi mwaka huu, huku ikilazimika kutoa maelezo kuhusu ujenzi wa reli ya kisasa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, alisema bungeni jana kuwa kanuni ya mafao itaanza kutumika Ijumaa ijayo na kwamba ndiyo yenye uhalisia.

Alisema kabla ya kuunganisha mifuko ya GEPF, LEPF, PSPF na PPF, kulikuwa na kanuni tofauti za mafao za GEPF, PPF na NSSF na wafanyakazi walioajiriwa baada ya 2014 walikuwa wanatumia kanuni inayowapa mkupuo wa asilimia 25 na wastani umri wa kuishi miaka 12.5.

Alisema wanachama wa mfuko wa PSPF na LEPF walikuwa wanalipwa mkupuo wa asilimia 50 na wastani wa umri wa kuishi miaka 15.5 na baada ya kanuni mpya zililenga kuweka uwiano wa mafao kwa wote.

Alisema serikali ilisikia kilio cha watumishi na kusitisha matumizi ya kikokotoo na kuunda kamati ili kuchambua uwezo, uhimilivu na uendelevu wa mifuko, kazi iliyofanyika tangu mwaka 2019 na makubaliano yamefikiwa kuanzia Julai Mosi, kanuni ya mafao kwa watumishi wote itakuwa asilimia 33.

**ATHARI YA ASILIMIA 50**

Waziri Ndalichako alitoa mfano kuwa mfanyakazi aliyechangia NSSF na mashirika ya umma aliyechangia miezi 350 kiasi cha Sh. milioni 86 kwa mafao kwa mkupuo wa asilimia 25 anapata Sh. milioni 54.

Waziri huyo alisema kwa kikokotoo kipya cha asilimia 33 mkupuo wa aliyechangia Sh. milioni 36 atapata Sh. milioni 71 na pensheni ya mwezi ni Sh. milioni 1.084 hadi atapofariki.

"Fomula iliyokuwa inawapa asilimia 50 haikuwa na uhalisia, ilisababisha hali ya uhimilivu na ukwasi wa mifuko kuendelea kupungua mwaka hadi mwaka na imejidhihirisha kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), alisema makusanyo ya wanachama ni madogo kuliko mafao yanayolipwa," alisema.

**WIZARA YA UJENZI**

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema ujenzi wa reli ya kisasa SGR waliachana na mchakato wa zabuni ya wazi kwa kuwa walipotangaza hawakupata mkandarasi na ndiyo maana walihamia kwenye mzabuni mmoja yaani 'single sourcing'.

Prof. Mbarawa alisema kipande cha nne cha reli hiyo walimpa mkandarasi aliyejaza bei kubwa ya Dola bilioni 1.498 sawa na dola milioni tisa kwa kila kilomita moja na waliamua kwenda kwenye 'single source', na walimpa nyaraka akajaza Sh. trilion 2.3 kwa kilomita 160 na wataalamu walikaa na kuona amekidhi vigezo.

Alisema walitumia miezi mitano kumpata kwa ajili ya kukubaliana ambaye alishusha bei kutoka Sh.trilioni 2.33 hadi trilioni 1.93 ikiwa ni punguzo la Sh. bilioni 406 sawa na asilimia 22.

**MIKOPO HALMASHAURI**

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema wamelazimika kupitia upya mapendekezo ya kupunguza mikopo ya halmashauri kwenda kwenye makundi maalum na sasa itaendelea kuwa asilimia 10 badala ya asilimia tano waliyopendekeza awali.

**KODI MIAKA 18**

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, alisema wamepokea ushauri wa wabunge wa kuendelea kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu kwa kila mwenye kipato mwenye umri wa miaka 18 kulipa kodi kwa kuwa na namba ya mlipakodi (TIN).

"Tunaomba wabunge waendelee kuwaelimisha wananchi ili kutambua uwezo wa vijana na siyo lazima walipe kodi kwa sababu ana TIN, tunataka ukiingiza NIDA kwenye mfumo inaonyesha taarifa zako zote," alisema.

# Polisi apigwa risasi kifuani akijihami

**Na Romana Mallya**

WATU watatu wanaodhaniwa majambazi, wameuawa na Jeshi la Polisi huku askari wake mmoja akijeruhiwa kwa risasi chini ya bega wakati wa majibizano na kundi la wahalifu hao lililovamia duka la bidhaa Goba, Tegeta A, Wilaya ya Ubungo mkoani Dar es Salaam jana mchana.

Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alikiri kutokea kwa tukio hilo jana saa 6:45 mchana kwenye duka la miamala ya fedha lijulikanalo kama Skymart Min Supermarket, watuhumiwa wanne wa ujambazi wakidaiwa kuvamia wakiwa na silaha.

Alisema walikuwa na silaha mbili aina ya Long Rifle 22 iliyotengenezwa Ubelgiji yenye risasi 11 pamoja na bastola aina ya Star yenye risasi sita, nondo na kisu. Kamanda Muliro alisema askari namba F3625 SGT Eliamini alijeruhiwa kwa risasi chini ya bega karibu na kifua na hali yake kiafya ilikuwa inaendelea kuimarika.

"Uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa kati ya watuhumiwa hawa wa ujambazi, wawili wametambuliwa majina yao ni Ridhiwani Mgeni, maarufu Babu Ally, aliyewahi kushtakiwa kwa kesi ya mauaji PI 148/2006 na Rajabu Ramadhan, maarufu Rogers, aliyewahi kushtakiwa kwa mauaji PI 28/2014," alisema.

Akisimulia tukio hilo, Kamanda Muliro alisema watuhumiwa hao walikuwa na pikipiki namba MC469 CMT aina ya TVS na walifika maeneo hayo kwa lengo la kuvamia na kupora fedha katika duka hilo lakini taarifa za haraka zililifikia Jeshi la Polisi.

"Polisi walipofika, majambazi walibaini 'hawa ni polisi makachero', walianza kufyatua risasi ovyo na moja ya risasi ilimjeruhi askari wetu chini ya bega karibu na kifua.

"Majambazi watatu walishambuliwa na kujeruhiwa vibaya wakawa kwenye hali mbaya na walipelekwa haraka hospitalini lakini walipoteza maisha na mmoja wao alitoroka,"alisema.

Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi linaendelea kufuatilia makundi yote yanayojihusisha na kupanga njama na kujaribu kutekeleza vitendo vya kihalifu.

# Watatu wapanda kizimbani madai ya uhujumu uchumi

**Na Grace Gurisha**

WAFANYABIASHARA watatu wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakikabiliwa na mashtaka 13 likiwamo la kuisababishia hasara ya Sh. bilioni 10 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kukwepa kodi.

Washtakiwa hao ni Joseph Msaki (35), Gift Msaki (40), Constantine Roman (38) , wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, ambao walisomewa mashtaka yao jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ramadhani Rugemalira

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali kutoka TRA, Medalakini Godwin, alidai kuwa washtakiwa hao walitenda makosa hayo kati ya Januari 2018 na Juni 15,2022 jijini Dar es Salaam.

Katika kesi hiyo, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashitaka manne ya kukwepa kodi, kutoa risiti za mashine za EFD zisizo halali, matumizi yasiyo sahihi ya mashine nne za EFD na shitaka moja la kuisababishia TRA hasara.

Godwin alidai katika shtaka kukwepa kodi washtakiwa hao wanadaiwa katika tarehe isiyofahamika kati ya Januari,2018 hadi Juni 15, 2022 jijini Dar es Salaam kwa pamoja wakiwa na nia ovu walijihusisha kutoa risiti isiyo halali kwa kutumia mashine ya EFD yenye jina la Romani Shirima.

Alidai mashine hiyo ilikuwa na mauzo ya Sh. 18,668,611,770 na matokeo yake walisababisha ukwepaji kodi ya ongezeko la thamani ya Sh. 5,580,002,499.

Pia, washitakiwa hao wanadaiwa kukwepa kodi kwa kutumia mashine ya EFD iliyosajiliwa kwa jina la Ahmada Ally na kusababisha ukwepaji kodi wa Sh. 784,734,295 huku mashine hiyo hiyo ikisababisha tena ukwepaji wa kodi ya Sh 582,551,181.

Katika shitaka la kutoa risiti isiyo sahihi, alidai kuwa katika kipindi hicho washitakiwa hao walitoa risiti isiyo sahihi kwa kutumia mashine ya EFD iliyosajiliwa kwa jina la Ahmada Ally wakati mashine hiyo ikiwa na taarifa ya mauzo ya Sh. 2,622,040,982 na kusababisha ukwepaji kodi wa shilingi 784,734,295.

Katika shitaka la matumizi yasiyo sahihi ya mashine ya EFD, alidai kuwa kati ya Januari 2018 hadi Juni 2022 kwa pamoja washtakiwa walitumia mashine hiyo isiyo sahihi yenye jina la Ngalasoni Shirima ambayo ilikuwa na mauzo ya shilingi 18,668,611,770,

Alidai kuwa walifanya hivyo kwa nia ya kumdanganya Kamishna Mkuu wa TRA na matokeo yake walikwepa kodi ya ongezeko la thamani ya Sh 5,580,002,499.

Katika shitaka la kuisababishia mmlaka hasara, inadaiwa kati ya Januari 2018 hadi Juni, 2022 jijini Dar es Salaam, wafanyabiashara hao kwa pamoja kwa nia ovu, walikwepa kodi na kusababisha TRA kupata hasara ya Sh. 10,507,755,190 . Baada ya washtakiwa hao kusomewa mashitaka yao, upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado unaendelea.

Hakimu Rugemalira aliwaeleza kwamba mashtaka yao ni ya uhujumu uchumi, Mahakama ya Kisutu haina mamlaka ya kusikiliza kesi yao, hivyo hawatatakiwa kujibu ndiyo au hapana. Pia, aliwaeleza kuwa kwa kiwango cha fedha kilichopo kwenye hati ya mashtaka, wanatakiwa kuomba dhamana yao Mahakama Kuu.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Julai 8,2022 na washtakiwa walipelekwa mahabusu.

"Utaratibu ulivyo ni kwamba washitakiwa wanatakiwa wakiletwa mahakamani upelelezi uwe umekamilika, kwa hiyo Julai 8, mwaka huu muwe mmekamilisha upelelezi," aliagiza hakimu huyo.

# LHRC yaja na mapendekezo Katiba Mpya

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimetoa mapendekezo manne kwa serikali kikiamini yatasaidia kufanikisha urejeshwaji wa mchakato wa Katiba Mpya.

Mapendekezo hayo yalitolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo hicho, Anna Henga, alipozungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam.

Pendekezo la kwanza ni serikali kupeleka muswada bungeni wa Mabadiliko ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ili kuunda upya Bunge Maalum la Katiba likiwa na uwakilishi wa wajumbe, tofauti na wabunge wachache wa vyama.

Kituo hicho pia kinapendekeza serikali kupeleka bungeni Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Kura ya Maoni ili kuipa uhalali wa kisheria, sheria hiyo.

Pendekezo la tatu ni Bunge Maalum la Katiba litakaloundwa, litumie Rasimu ya Pili ya Katiba katika majadiliano huku kituo hicho kikiwa pendekezo la nne la kuitaka serikali iendelee kufungua milango ya majadiliano miongoni mwa Watanzania kwa njia ya mikutano, makongamano, midahalo na vyombo vya habari juu ya mambo ya msingi na muhimu ndani ya Katiba kwa mustakabali wa Taifa.

"Kituo cha Haki za Binadamu kinapongeza uamuzi uliofanywa NEC ya Chama Cha Mapinduzi CCM kuridhia kufufua mchakato wa Katiba Mpya, kulingana na taarifa iliyotolewa na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema uamuzi huo ni ishara nzuri ya kuimarisha demokrasia na haki za binadamu nchini, ambapo kituo hicho kimempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa hatua hiyo.

"Kulikuwa na mabishano ya muundo wa serikali, hoja ya kuwa na serikali moja au mbili, ambapo jambo hilo lilisababisha hoja nyingine kutojadiliwa ambapo pia zina umuhimu katika jamii," alisema Anna alipokumbusha yaliyojiri kwenye Bunge Maalum la Katiba.

Alisema, LHRC inatoa maoni ya namna bora ya kuendelea na mchakato ikiwamo kufanya mabadiliko ya sheria yote ya Mabadiliko ya Katiba Na. 8/211 na kuweka muundo mpya wa Bunge Maalum la Katiba, ili kuanza majadiliano ya kutunga Katiba Mpya.

"Bunge hilo litumie Rasimu ya Pili ya Katiba. Hii inatokana na ukweli kwamba kulikuwa na mjadala mkali kuhusu upatikanaji wa Katiba Pendekezwa mwaka 2014," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, mkoani Dar es Salaam jana, wakati akitoa maoni ya kituo hicho kuhusu namna bora ya kufufua mchakato wa Katiba Mpya. Kulia ni Ofisa Uchechemuzi wa kituo hicho, Maduhu William na Mkurugenzi wa Ujengaji Uwezo na Uwajibikaji, Felista Mauya. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Acharuka wananchi kutosomewa mapato

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

MKUU wa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Jerry Muro, amewaagiza viongozi wa vitongoji, vijiji na kata kujenga utamaduni wa kusikiliza kero za wananchi, kuitisha mikutano na kuwasomea mapato na matumizi kama taratibu na sheria zinavyoelekeza.

Alitoa agizo hilo jana kwenye mkutano wa madiwani, wenyeviti wa vijiji, watendaji wa vijiji na wenyeviti wa vitongoji vya Kata ya Puma, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake kusikiliza kero na namna ambavyo viongozi wa maeneo husika wamewajibika kuzipatia ufumbuzi.

Muro alisema ni aibu kwa mwenyekiti wa kijiji au kitongoji tangu achaguliwe hajawahi kuitisha mkutano wa hadhara kuwasomea mapato na matumizi ya kijiji wananchi wake kwa kuwa hiyo ndiyo inawapa wakati mgumu wakati wa uchaguzi.

"Baadhi ya viongozi wanatoa visingizio kuwa wakiitisha mikutano wananchi hawaji, kama ukiona mwenyekiti unaitisha mkutano hawaji, basi ujue wewe una tatizo na sasa unatakiwa kurudi ndani ujiulize wewe na mtendaji wako mtafakari kuna nini, maana haiwezekani waliokuchagua wakashindwa kukusikiliza," alisema. Muro alisema viongozi lazima watambue kuwa ukiwahudumia wananchi kwa kutatua kero zao, ni lazima wakati wa uchaguzi watakupa kura na kama husikilizi shida zao, ikifika kwenye uchaguzi wanakupiga chini.

"Tunahitaji kuona viongozi wanakwenda kusikiliza kero za wananchi, wanakagua miradi ya maendeleo, miradi hii ni ya kwenu, siyo ya DC (mkuu wa wilaya)," alisema.

Muro alisema staili ya utendaji wake wa kazi ni kuwajengea mfumo wa utendaji kwa kuwa siyo vizuri kila kero hadi afike mkuu wa wilaya kuitatua.

"Kiongozi mzuri ni yule anayetengeneza mfumo wa idara yake ili mfumo ufanye kazi na siyo yeye, mfumo ukifanya kazi hata yeye kichwa kitapungua, lakini ikiwa kila kitu DC mwisho wa siku ikifika wakati wa uchaguzi utataka aje akuombee kura, sababu kazi amefanya yeye," alisema.

Katika mkutano huo, Muro alipata fursa kusikiliza kero mbalimbali na kuzitatua papo hapo.

Miongoni mwa kero ilikuwa ni mradi wa urasimishaji wa ardhi ambao baadhi ya wananchi walilipia gharama za kupimia lakini zoei limekwama tangu mwaka 2018. Kutokana na shida hiyo, Mkuu wa Wilaya alimwagiza Ofisa Ardhi na Maliasili Wilaya ya Ikungi, Ambroce Ngonyani, kuhakikisha uwekaji alama za mipaka unaanza mara moja katika maeneo ambayo tayari mchakato ulishakamilika.

# Meli kubwa iliyobeba mbolea yawasili nchini

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

MELI Kubwa Iliyobeba viuatilifu aina salfa tani 5,623 imetua salama katika Bandari ya Mtwara ikitokea Jeda, Saudi Arabia.

Meli hiyo aina ya 'boss seven' iliyopokea mzigo kutoka Uturuki ikiwa na viuatilifu hivyo, imefika mahali hapo tayari kwa kupakuliwa na kuanza kwa mchakato wa kuvigawa kwa wakulima.

Meneja wa Bandari hiyo, Norbert Kalembwe, alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari mjini hapa kuhusu faida za viatilifu hivyo kwa wakulima.

Alisema viatilifu aina ya salfa vilivyomo katika meli hiyo vitakuwa msaada mkubwa kwa wakulima wa korosho, akibainisha vitasaidia kuinua uchumi kwa wakulima hao.

"Meli hii imefika na viuatilifu salama na sasa kilichobaki ni kuhakikisha kwamba vipo katika ubora unaotakiwa na baada ya kufanya hilo, ndipo tutaanza mchakato wa kuvigawa kwa wakulima.

"Hivi viuatilifu ni vya gharama kubwa, hivyo serikali inastahili pongezi kwa sababu kwa wakulima wa korosho, salfa ni dawa muhimu sana," alisema.

Mkurugenzi Bodi ya Korosho, Francis Alfred, pamoja na Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Aloyce Mwanjire, kwa pamoja walimshukru Rais Saimia Suluhu Hassan, kwa kutoa viuatilifu hivyo bila malipo kwa wakulima ili waweze kutibu mazao yao.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa moyo wake wa huruma kwa kututazama sisi wakulima wa korosho, Kwa leo (jana) tunapokea salfa ya unga, hii ni dawa ya kutibu ugonjwa wa bwiliunga na ukifanikiwa kutibu ugonjwa huo kwa zao la korosho, lazima utapata kipato kikubwa na hali hiyo itaongeza kipato na upatikanaji wa kodi," walisema

Pia waliwakumbusha wakulima wa korosho kuacha kubweteka na msaada unaotolewa na Rais na kuwasistiza wanapovuna mazao yao wakumbuke kutenga pesa kwa ajili ya kununua pembejeo za kilimo.

Mkuu wa Mkoa huo, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, aliagiza watu wote watakaohusika katika ugawaji wa pembejeo hizo kuzigawa kwa wakati na bila upendeleo ili kila mkulima afaidike na pembejeo hizo.

"Namhakikishia Rais wetu mpendwa, pembejeo hizi zimefika mahali pake, wakulima wa zao hili wamefurahi sana kuona ametoa tani 5,623 kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wa zao la korosho.

"Kwa hiyo, ninataka niseme wale wote watakaopewa nafasi ya kugawa pembejeo hizi, wakazigawe kwa umakini mkubwa, hatutasita kumchukulia mtu hatua pale tutakapobaini hali ya ubadhirifu katika pembejeo hizi," alionya.

Pia aligusia kuwa mwaka uliopita aliwaweka ndani wafanyakazi 12 wakiwamo waajiriwa wa serikali kwa kosa la ubadhirifu wa pembejeo hizo za kilimo na kutoa msisitizo hataki kuona hilo likijitokeza.

## Waandaa kampeni kuhamasisha sensa

**Na Mary Geofrey**

ASASI ya Wanawake nchini ya Promoting Women's Empowering for Better Health Out coming (PROWEBHO), imendaa kampeni ya uhamasishaji wa sensa ya watu na makazi kwa kutumia nyenzo mbalimbali zenye nembo ya sensa.

Mkurugenzi Mtendaji wa PROWEBHO, Catherine Sembua, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, kuhusu kampeni hiyo alisema itafanyika kwenye mikoa mitano ya Mwanza, Dar es Salam, Dodoma, Lindi na Zanzibar.

Alisema watagawa stika, kalamu, opena, viholda vya funguo, tisheti, kofia, vitambaa vya mkononi na vipeperushi kuanzia ngazi ya vijiji, vitongoji, mitaa, kata, wilaya, shuleni, kwenye vyombo vya usafiri, vituo vya mabasi na maeneo yote ya mikusanyiko.

"PROWEBHO Tanzania kwa kuitikia wito wa Rais Samia Suluhu Hassan, imejipanga kufanya uhamasishaji kwa kutumia nyenzo mbalimbali zitakazobeba ujumbe wa sensa pamoja na kuonyesha tarehe ya kuhesabiwa.

"Tutafanya pia uhamasishaji na uelimishaji kwenye makundi ya watu wenye uhitaji maalum wakiwamo wenye ulemavu wa ngozi na kutosikia na waathirika wa dawa za kulevya," alisema Catherine.

Alisema umuhimu wa sensa ya watu na makazi ni kupata takwimu sahihi zitakazowezesha serikali na wadau wengine kupanga kwa usahihi mipango ya maendeleo ya watu wake, katika sekta zote ikiwamo elimu, afya, maji safi, nishati, hali ya ajira na uwezeshwaji wa makundi yenye uhitaji maalum.

"Ili kuhakikisha zoezi hili linakuwa na mafanikio makubwa PROWEBHO inatoa wito kwa wananchi kujitokeza na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa makarani wa sensa watakapotembelea katika kaya zao kwa kujibu maswali yote yatakayoulizwa," alisema Catherine.

Alisema uzinduzi rasmi na nyenzo hizo utafanyika Julai katika mkoa wa Dar es Salaam na Agosti 16, jijini Dodoma.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam, Hassan Rugwa, aliipongeza asasi hiyo kwa juhudi kubwa wanazofanya kuiunga mkono serikali. Kadhalika, aliwataka wananchi kutumia nyenzo hizo kujikumbusha kuhusu tarehe ya kuhesabiwa, pia kushiriki kikamilifu ili kulisaidia taifa kuwa na takwimu sahihi ambazo zitarahisisha utoaji wa huduma.

# TACAIDS yaandaa mkakati wa kumaliza Ukimwi kufikia 2030

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) ipo kwenye maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa Tano wa Kudhibiti Ukimwi (NMSF V) utakaochangia kumaliza tatizo hilo ifikapo mwaka 2030.

Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, alibainisha hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa kikao cha Kamisheni ya Tume hiyo na Bodi ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti Ukimwi (ATF) ili kujadili mkakati huo.

Alisema mkakati huo ni mwongozo wa kitaifa katika utekelezaji wa shughuli za Ukimwi ili kuendena na mikakati ya ndani na ya kidunia ikiwa ni pamoja na Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Ukimwi mwaka 2020/2021, Mkakati wa Dunia wa Ukimwi (GIS) na Mkakati wa Sekta ya Afya na Sera ya Sekta ya Afya ya Mwaka 2020.

Mwezeshaji kiongozi wa mkakati huo, Dk. Emmanuel Matech, alisema mkakati huo umeainisha sekta zote kuja pamoja katika msukumo wa pamoja kuhakikisha kila moja inachangia katika jitihada za kumaliza Ukimwi ifikapo 2030.

"Mkakati huu tunahitaji sekta zote zije pamoja katika kumaliza Ukimwi, hivyo sekta zote zinahitaji msukumo wa pamoja katika utekelezaji na mkakati huu unaonyesha kila sekta itafanya nini katika utekelezaji au inachangia vipi katika kumaliza Ukimwi," alisema.

Alitaja baadhi ya maeneo ya vipaumbele vya mkakati huo ni maambukizo mapya, matibabu, upimaji, kuondoa maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto, kuondoa vikwazo pamoja na kutokuwa na usawa, kuwa na uhakika na huduma zikisaidiwa na mipango au mifumo imara pamoja na kuimarisha utendaji na uhakika wa rasilimali pamoja na ufuatiliaji na tathmini.

Wakichangia katika kikao hicho, wajumbe wa Bodi ya ATF na Kamisheni ya TACAIDS, walisema jitihada zimefanyika katika uandaaji wa mkakati huo japo upo upungufu mdogo ambao unahitaji kufanyiwa marekebisho ikiwa ni pamoja na kuongoza eneo la uraghibishi kwa upande wa viongozi wa dini, afua ya mabadiliko ya tabia pia ni muhimu ionekane katika mkakati huu.



Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi Zanzibar, Suleiman Makame (kulia), akimpongeza mdau wa bahari wa muda mrefu, Ibrahim Bendera, wakati wa kufunga kongamano la uchumi wa bluu lililoandaliwa na Chuo cha Bahari (DMI), jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Watanzania wapewa fursa uchumi wa buluu

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imesema inaweka mazingira mazuri kuhakikisha kipaumbele kwenye fursa zilizoko kwenye uchumi wa buluu kinakuwa kwa Watanzania kabla ya wageni kunyakua fursa hizo zinazopatikana kwenye bahari.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Suleiman Makame, wakati akizungumza kwenye ufungaji wa kongamano la siku mbili la uchumi wa buluu, lililoandaliwa na Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI). Alisema iwapo Watanzania wengi watachangamkia fursa hizo na kuzitumia kwa uzalishaji, fedha zitakazopatikana zitawasaidia kwa maendeleo na kubaki kwenye mzunguko wa uchumi tofauti na iwapo fursa hizo zitachukuliwa na wageni.

"Kwa muda mrefu tumeona meli za uvuvi za kigeni zikivua kwenye bahari yetu zikichukua rasilimali zetu zilizoko baharini na sisi kubaki kuwa watazamaji mimi nadhani huu ni wakati wa kujipanga ili tuzitumie wenyewe kwasababu uwezo huo tunao," alisema.

Aliutaka uongozi wa Chuo cha Bahari (DMI), kuboresha mitaala yake na kufundisha kozi ya ubaharia wa uvuvi kwa kuwa kuna meli nyingi za uvuvi zinakuja ambazo zitahitaji wataalamu.

Alisema miezi mitatu iliyopita serikali ilipokea meli ya uvuvi wa bahari kuu na kuna uhitaji wa mabaharia wazalendo wa uvuvi ambao watahudumia meli hiyo na zingine zinazokuja badala ya kutegemea wataalamu wa kigeni.

"Mimi siyo baharia ila nimekaa sana na mabaharia, wengi ninao wajua sio mabaharia wa uvuvi, wengi ni manahodha wa meli, wahandisi wa meli sasa mkuu wa chuo cha DMI kwenye mitaala yako weka hii ya uvuvi wa bahari tuzalishe wataalamu wetu wenyewe," alisema.

Waziri alifafanua kuwa Watanzania wengi bado hawajaitumia bahari ipasavyo kwa kuendelea kufanya uvuvi mdogo na kwamba kuna haja ya kubadilika na kwenda kufanya uvuvi kwenye bahari kuu ili kuchangia ukuaji wa uchumi kwa kuwa huko ndiko wanapatikana samaki wengi.

"Sisi Zanzibar tumeshaanza kujipanga kwenda kwenye uvuvi wa bahari kuu sasa na nyinyi mjipange msiendelee kuwa watu wa kutoa vibali vya uvuvi kwa wageni na kubaki kuwa wasindikizaji wakati rasilimali zinazidi kuchukuliwa na wageni, tubadilike kama tulivyobadilika kwenye madini," alisisitiza waziri.

Aliwataka washiriki kwenda kutekeleza kwa vitendo yale waliyojifunza kwenye kongamano hilo la siku mbili na kuwaelimisha watu ambao hawakupata fursa ya kuhudhuria fursa zinazopatikana baharini. "Tumekaa hapa kwa siku mbili na tumeelezwa nini maana ya uchumi wa buluu na fursa zinazopatikana baharini sasa kinachofuata ni kutekeleza kwa vitendo kuhakikisha nchi yetu inanufaika ipasavyo na bahari na vilivyomo ndani yake tusiwachie wageni," alisema.

Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Dk. Tumaini Gurumo, alisema chuo hicho kwa muda mrefu kinatoa mabaharia ambao sio wa uvuvi na kimechukua ushauri wa waziri na kitaweka mazingira ya kuwafundisha mabaharia hao.

"Tunafahamu kwamba uendelezaji wa rasilimali wa uvuvi ni muhimu sana katika kuufikisha uchumi wa buluu pale ambapo serikali inataka kuufikisha hivyo maagizo ya waziri tumeyapokea na tunaenda kuyatekeleza," alisema.

Alisema ni kweli kwa muda mrefu sasa Watanzania wengi wanafanya uvuvi mdogo wa kujikimu usiokuwa na tija kwao hivyo kwa dhana ya sasa ya uchumi wa buluu serikali inataka wananchi wabadilike na waachane na uvuvi wa kujikimu na waende bahari kuu.

"Kuna watu wanaishi kando ya bahari, lakini wamezoea uvuvi wa mlo wa siku unakuta mtu amezoea akiamka asubuhi anaenda kuchukua samaki kidogo hapo kusogeza maisha sasa hayo tunataka kuachana nayo twende mbali zaidi," alisema.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wachezaji epukeni usajili unaofaidisha timu pekee

**LIGI** Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/ 2022 inatarajia kufikia tamati Juni 29, mwaka huu kwa timu zote 16 zinazoshiriki ligi hiyo kushuka dimbani kusaka pointi tatu muhimu.

Hata hivyo wakati ligi hiyo ikielekea ukingoni tayari bingwa mpya ameshapatikana naye si mwingine ni klabu ya Yanga ya jijini Dar es Salaam.

Yanga iliwavua mabingwa mara nne mfululizo, Simba wiki iliyopita baada ya kufikisha pointi ambazo haziwezi kufikiwa na timu nyingine, hapo ilikuwa na mechi tatu mkononi.

Kwa heshima ya kutwaa taji hilo, Yanga inayofundishwa na Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi, itakabidhiwa kombe lake leo kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya baada ya kumalizika kwa mechi ya raundi ya 29 dhidi ya wenyeji Mbeya City.

Hii inamaanisha kwamba vita iliyobakia katika mechi za hatua ya lala salama ni ya kusaka tiketi mbili za kushiriki mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), zilizobakia baada ya Simba iliyoko kwenye nafasi ya pili tayari kupata nafasi hiyo kutokana na pointi zake 60 ilizonazo. Vita hiyo inaweza tu isiwe na kusaka tiketi ya kushiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, lakini ikawa ni kusaka zawadi ya fedha zitakazotolewa na wadhamini wa ligi hiyo, Kampuni ya Azam Media ambao msimu huu watatoa bonus hadi kwa timu itakayoshuka daraja.

Kwa kifupi, vita iliyopo au michezo ambayo itakuwa na ushindani au inayotakiwa kuangaliwa kwa jicho la tatu ili kuepuka upangaji matokeo ni ile inayohusisha timu zilizoko kwenye janga la kushuka daraja.

Kumalizika kwa msimu huu ndio ishara sahihi ya kuanza kwa maandalizi ya msimu mpya wa 2022/2023. Tayari Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ambalo liko chini ya Rais, Wallace Karia na Katibu Mkuu, Wilfred Kidao, limeshatangaza dirisha la usajili litafunguliwa rasmi ifikapo Julai Mosi na kufungwa Agosti 31, mwaka huu.

Lakini pia likiweka wazi usajili wa dirisha dogo utafanyika kuanzia Desemba 16, mwaka huu hadi Januari 15, mwakani. Klabu zimetakiwa kutumia muda huo kukamilisha usajili mpya na taratibu za uhamisho kwa nyota wote na ukihusisha timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Championship, First League na Ligi Kuu ya Wanawake.

Kuelekea mchakato huu, wachezaji na timu zimeshaanza kufanya mazungumzo ya kusaini mikataba huku wengine wakiwa tayari wamekamilisha mazungumzo hayo na kuanza kutambulishwa.

Mara nyingi wachezaji ndio wamekuwa wahanga wakubwa wa mazungumzo hayo kwa kusaini mikataba ambayo inawapa upendeleo klabu na kuwaweka kifungoni wao, hasa pale wanapotaka kuondoka na kujiunga na klabu nyingine ama kwa kupata ofa nono au kujaribu changamoto mpya baada ya kuishi klabu moja kwa muda mrefu.

Umefika wakati wachezaji kupitia mawakala, mameneja, wazazi au walezi wao wanaowasimamia kuwa makini na mikataba inayolenga kuwaumiza wachezaji na hivyo kuonekana kama mikataba ile ya wakoloni ambayo iliwaumiza babu zetu. Wachezaji mnatakiwa kuhusisha mawakala au wanasheria kabla ya kusaini mikataba ili kujiweka mahali salama na kujiepusha na hatua za kufungua kesi baada ya kubaini klabu iliweka vipengele tata kwenye mkataba ambao ulisaini na hivyo kukuwekea ugumu pale unapopata fursa mpya.

Viongozi wa klabu watendeeni haki wachezaji kwa kuacha tabia ya kuwabana au kuwawekea ngumu vijana wenu hasa pale wanapopata ofa kwa klabu nyingine/ zingine za ndani au nje ya nchi.

TFF pia iendelee kuwasimamia wachezaji hasa wazalendo kwa sababu wanapopata changamoto ya kuachwa au kunyimwa baraka za kujiunga na timu nyingine, vitendo hivyo vinachangia kurudisha nyuma vipaji vyao na hali hiyo kuigharimu nchi kwa kushindwa kuitwa kwenye timu za taifa pale wanapohitajika.

Tunawakumbusha wachezaji pia kuacha kukurupuka kusaini mikataba bila ya kuelewa vipengele lakini pia kutoweka mbele maslahi hali ya kuwa hawana uhakika wa kupata namba kwenye kikosi cha kwanza katika timu mpya inayowasajili na hivyo kuchangia kuua kipaji chake mwenyewe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

### Adhabu Biashara United funzo kwa timu nyingine

Na Adam Fungamwango

**HIVI** majuzi Kamati ya Nidhamu ya Shirikisho la Kimataifa la Mpira wa Miguu (FIFA) imeishushia rungu klabu ya Biashara United kusajili mchezaji yoyote mpya kwa madirisha mawili.

Ina maana klabu hiyo haitosajili kwa msimu mzima wa 2022/23, kwenye dirisha kubwa linalotarajiwa kuanza Julai Mosi hadi Agosti 31 mwaka huu, na ule wa dirisha dogo ambao unatarajiwa kuwa Desemba 16 mwaka huu hadi Januari 15 mwakani.

Shirikisho la Soka Nchini (TFF) likasema adhabu hiyo imetolewa baada ya timu hiyo kushindwa kuheshimu uamuzi wa awali wa FIFA kuifungia kusajili wachezaji hadi itakapokamilisha malipo ya madai ya mishahara ya aliyekuwa mchezaji wake, Timoth Balton Omwenga.

Kutokana na kutoheshimu uamuzi huo, ndipo FIFA ilipowasilisha suala hilo kwenye kamati yake ya nidhamu ambayo Mei 19, mwaka huu ilitoa adhabu hiyo kupitia mjumbe wake, Carlos Teran wa Venezuela.

Hili ni pigo zito kwa Biashara United ambayo tayari ipo hoi bin taaban katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa inashika nafasi ya 15 kati ya timu 16 zinazoshiriki ligi hiyo. Inapigania uhai wa kubaki Ligi Kuu, au hata kwenda tu kucheza mechi za mchujo 'play off''.

Kilichotokea ni kama vile mtu aliyebakisha nauli ya basi tu mfukoni, lakini hiyo hiyo baadaye nayo ikachukuliwa kwa kuibiwa au kupotea.

Ni huzuni iliyoje kwa timu hiyo ambayo msimu huu ilicheza michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika na ilikuwa bado kidogo itinge kwenye hatua ya makundi, kwani katika mechi ya kwanza hapa nchini iliichapa Al Ahly Tripoli ya Libya mabao 2-0, lakini kwa bahati mbaya au uzembe, ikashindwa kwenda katika mchezo wa marudiano ugenini.

Timu iliyofungwa na Biashara United na kusonga mbele kwa ushindi wa chee, ilifanikiwa kutinga mpaka hatua ya nusu fainali ya kombe hilo, ikitolewa na Orlando Pirates ya Afrika Kusini ambayo katika hatua ya robo fainali iliibwaga Simba.

Hapa unaweza kuona Biashara United ilikuwa ni timu iliyokamilika, lakini ukiangalia kwa makini ni kama imekosa viongozi bora.

Hata mechi za mwanzo za kombe hilo zilisafiri kwa kubahatisha, kabla ya kushindwa kwenda Libya.

Ibaki Ligi Kuu au ishuke daraja, Biashara United sasa itaendelea kuwa na wachezaji hao hao, ambao kwa ninavyolijua soka la Tanzania, baadhi yao msimu ujao watasajiliwa na klabu nyingine, tena kama ikishuka ndiyo kabisa wataondoka wengi, labda wale ambao hawatakiwi.

Nadhani watalazimika kuwapandisha wachezaji wengi wa chini ya miaka 20, sipati picha kama itabaki Ligi Kuu halafu uwe na vijana wa aina hiyo wengi kwenye timu.

Nilimsikia kiongozi wake mmoja akidai hawakujua kama ni usajili wa wachezaji wa ndani au wa nje.

Hii ni aina ya viongozi ambao hawajui hata kanuni na inapofanya kazi wanashangaa.

Mfano hivi sasa maoni ya wadau wa soka wanakusanywa ili kutengeneza kanuni ya msimu ujao wa ligi, cha ajabu unaweza kukuta baadhi ya viongozi wa klabu hawashiriki na wala hawazijui, ila watakuja kulalamika siku zikianza kufanya kazi na kuuma upande wao.

Viongozi wa TFF kupitia kamati zao sasa inabidi waendeshe semina kwa viongozi wa klabu, kwani ni aibu na kiongozi yoyote kuonekana kutojua chochote kuhusu kanuni za usajili, lakini hata klabu inapofungiwa, bado anakuwa haelewi.

Najua ingekuwa ni Simba au Yanga, zimefungiwa, lawama zingeenda zaidi TFF kuwa hadi viongozi hao wanasajili wao walikuwa wapi wasiwajulishe.

Imefika wakati kufungiwa Biashara United inawezekana kuonekana ni jambo dogo kwa baadhi ya mashabiki wa soka nchini, lakini hili ni somo na funzo kubwa kwa wadau wengine.

Tumekuwa na mlolongo wa taarifa za wachezaji na makocha kudai pesa zao kwenye klabu hata zile zinazoitwa au kujiita kubwa.

Tena unakuta wanadaiwa halafu wanajibu kwa jeuri na kujiamini. Inafaa waelewe FIFA huwa hawajali ukubwa wa timu na inapoamua kushusha rungu inashusha bila kujali mashabiki watasema nini. Wenyewe wanaangalia zaidi sheria inasemaje na si busara kama ambayo maamuzi yetu nchini yanavyokuwa wakati mwingine wa kisiasa.

Ni wakati sasa viongozi wa klabu kuendesha soka kisasa, kuwalipa wachezaji na waajiriwa wote mishahara kwa wakati na hata kama hawana, basi kuongea nao kirafiki, badala ya kuwajibu majibu yasiyoeleweka na kukimbilia FIFA.

Na hii imeonekana sana kwa wachezaji wa kigeni, wamekuwa wanajitambua sana na hasa kwenye kudai maslahi yao, tofauti na wachezaji wa Kitanzania ambao wanaona aibu kudai au wanaogopa.

Adhabu hii ambayo Biashara United imeipata kama viongozi wa klabu za soka hapa nchini hawatajirekebisha, basi tusishangae kuzikuta timu nyingine zikikumbana na rungu hili.

## ‘Hakuna mtaala somo la Historia’

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, amesema hakuna mtaala wa somo la Historia isipokuwa upo muhtasari wake.

Kipanga alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Chumbuni (CCM), Ussi Pondeza.

Mbunge huyo alihoji ushirikishwaji wa wataalamu kutoka Zanzibar katika kuandaa mtaala wa somo la Historia ili kuandikwa kwa usahihi ikizingatiwa kuwa historia ya Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara zipo tofauti.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kipanga alisema uandaaji wa muhtasari wa somo la Historia ya Tanzania ulishirikisha wataalamu na wadau kutoka Zanzibar kwa kila hatua ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi.

Aliwataja wataalamu na wadau hao ni pamoja na Taasisi ya Elimu Zanzibar, State University of Zanzibar (SUZA), SUMAIT University, Chuo cha Kiislamu Mazizini (CCK), watu mashuhuri na viongozi wastaafu.

## Miradi 180 ya maji sasa yakarabatiwa

SERIKALI imesema katika mwaka wa fedha 2021/22 miradi ya maji 181 imekarabatiwa.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Husna Sekiboko.

Mbunge huyo alihoji lini serikali itaanza kutoa ruzuku ya ukarabati wa miradi ya maji kama inavyofanya kwa miradi ya barabara.

Akijibu swali hilo, Mahundi alisema serikali ina utaratibu wa kila mwaka wa fedha kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa miradi ya maji ili iendelee kutoa huduma iliyokusudiwa mijini na vijijini.

“Katika mwaka wa fedha 2021/22 miradi 181 imekarabatiwa. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, serikali itaendelea na ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji katika maeneo mbalimbali nchini,” alisema.

Katika Swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji lini serikali itaweka fedha ya kukarabati miradi ya maji badala ya kusubiri iharibike kwanza.

Alisema kuna utaratibu wa wale wataalamu wanaokarabati miradi vijijini wanalipwa na kamati za maji, jambo ambalo ni mzigo mzito kwa wananchi na kuhoji lini serikali itawaajiri na kuwalipa ili wasiwe mzigo kwa wananchi.

Akijibu swali hilo, naibu waziri huyo alisema kwa mwaka ujao wa fedha, serikali imetenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa miradi ya maji.

Alisema wizara inaendelea kuwafuatilia wataalamu wake kwenye mikoa na wilaya ili kutimiza majukumu yao na fedha zimetengwa kwa ajili kuajiri wataalamu hao.

# Wizara kukarabati jengo la kihistoria

WIZARA ya Maliasili na Utalii imesema serikali itaendelea kushirikiana na familia ya Chifu Adam Sapi Mkwawa kuona namna nzuri ya kulikarabati jengo aliloishi la kihistoria.

Naibu Waziri wake, Mary Masanja, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kalenga (CCM), Jackson Kiswaga.

Mbunge huyo alihoji ni lini serikali itajenga barabara ya kwenda Kituo cha Makumbusho ya Mkwawa kwa kiwango cha lami pamoja na kukarabati jengo aliloishi Chifu Adam Sapi Mkwawa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Masanja alibainisha kuwa kutokana na umuhimu wa barabara hiyo, wizara itaendelea kushirikiana na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Iringa kuitunza na kuifanyia ukarabati barabara hiyo ili ipitike kwa vipindi vyote.

Alisema jengo aliloishi Chifu Adam Sapi Mkwawa lipo nje ya mipaka ya hifadhi ya Kituo cha Makumbusho ya Kalenga yapata kiasi cha mita 250 na linaendelea kutumiwa na wanafamilia na kwamba serikali itakutana na familia kuona namna ya kulikarabati.

Katika swali lake la nyongeza, mbunge huyo alihoji lini serikali itakarabati miundombinu ya mapango ya Isimila ili kutumika kwenye utalii.

Masanja, akijibu swali hilo, alisema maeneo ya wapigania uhuru serikali inayatambua na ilishayaanisha na serikali itaendelea kufanya mazungumzo na wana familia kwa kuwa maeneo hayo kwa asilimia kubwa yalichukuliwa na wanafamilia.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (kulia), akijadiliana jambo na Mbunge wa Monduli, Fred Lowasa, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yatoa ufafanuzi gharama kubadili fedha

WIZARA ya Fedha na Mipango imesema mahitaji ya sarafu kubwa yapo juu zaidi kuzidi mahitaji ya sarafu ndogo, hivyo bei yake ya kununuliwa huwa juu.


Naibu Waziri wake, Hamad Hassan Chande, aliyasema hayo jana wakati akijibu swali la Mbunge wa Kinondoni (CCM), Tarimba Abbas.

Tarimba alihoji kauli ya serikali kuhusu shida iliyopo katika uuzaji na ununuzi wa fedha za kigeni nchini katika benki na maduka ya kubadilisha fedha kwa kulipa kima tofauti kwa noti za dola 100 na noti ndogo za dola 20, dola 10, dola tano na dola moja.

Akijibu swali hilo, naibu waziri huyo alisema fedha za kigeni zinapokuwa nchini, huchukuliwa kama bidhaa ambayo hutunzwa na kuuzwa kwa thamani tofauti.

Alisema gharama za kutunza sarafu ndogo ni kubwa kulinganisha gharama za kutunza sarafu kubwa.

“Mahitaji ya sarafu kubwa yapo juu zaidi kuzidi mahitaji ya sarafu ndogo, hivyo bei yake ya kununuliwa huwa juu,”alisema. Alisisitiza kulingana na gharama ya utunzaji, mahitaji na wepesi wa kuziuza, sarafu za dola za Marekani 100 na 50 hununuliwa kwa bei ya juu kuliko sarafu za Dola za Marekani 20, 10, tano na moja.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# Wananchi wapewa elimu kukabili tembo wavamizi

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

TATIZO la wananchi wanaoishi katika kata za Kyaitoke, Luhunga na Kibirizi Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, mkoani Kagera la kuvamiwa na tembo limeanza kupatiwa ufumbuzi, baada ya Shirika la Hifadhi za Taifa nchini (TANAPA), kuanza mchakato wa kupata fedha kuwahamisha tembo wanaokadiriwa 80 kuwapeleka hifadhini.

Akizungumza katika mkutano maalumu wa baraza la madiwani wa halmashauri ya wilaya hiyo, maofisa wa TANAPA walioalikwa kwa lengo la kutoa elimu ya wananchi kukabiliana na tembo wanaovamia makazi yao, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi kutoka ofisi za hifadhi za Taifa za Ibanda na Rumanyika, mkoani Kagera, Moronda Moronda, alisema ana imani fedha hizo zitapatikana na tatizo hilo kupatiwa ufumbuzi.

“Katika mipango ya muda mrefu tumepanga kujenga jengo la askari katika eneo la Kihanga, wilayani Karagwe, kutakuwa na askari sita ambao watakuwa wakikimbia kwenda kutoa msaada wa haraka, lakini la mwisho ni suala la kuwahamaisha kama itawezekana, tayari limekwishafikishwa kwa Waziri wa Maliasili na Utalii analifahamu,” alisema Kamishna Moronda.

Alisema tembo hao wakishahamishwa watafungwa kifaa maalum shingoni kitakachounganishwa na kompyuta kitakacho wabaini haraka na kuzuiliwa kutoka wanapojaribu kutoka hifadhini.

Naye Ofisa Uhifadhi Mkuu kutoka katika Ofisi za Hifadhi, Upendo Massawe, alisema tembo wanaovamia wananchi wa kata hizo hawatoki hifadhini, ndiyo maana wakifukuzwa kata moja wanakimbilia nyingine, na kuwataka wananchi kutumia njia za asili ikiwamo kupanda pilipili, tumbaku na ufuta kuzunguka mashamba yao, ili kuzuia wanyama hao kuingia katika mashamba yao.

“Unaweza kuchimba mtaro ambao tembo akiuona hataingia au akiingia hatoki, lakini pia unaweza kutumia vitambaa vyenye mchanganyiko wa oil chafu na pilipili, ukichanganya hivi vitu ukatengeneza uzio wa kitambaa kuzunguka shamba lako tembo hatakuja,” alisema Massawe.

Aidha,aliwataka wananchi kutohifadhi vyakula katika maghala yaliyo karibu na maeneo wanapolala ili kuepusha tembo kunusa na kuvamia, na kutovaa nguo zinazong’aa wanapofukuza tembo katika mashamba yao, kwa kuwa nguo hizo zinaweza kusababisha mnyama huyo kuwaona kwa urahisi.

Madiwani kutoka katika kata hizo tatu zilizoathiriwa zaidi na wanyama hao, Kijoma Kaijage wa Kyaitoke, Audason Audax wa Luhunga na Lameck Timanywa wa Kibirizi, waliomba zoezi la kuwahamisha tembo hao kufanyika haraka ili kunusuru maisha na mashamba ya wananchi wanaoishi katika kata hizo.

“Wananchi 16 kwenye kata yangu ya Kyaitoke nyumba zao tatu zimebomolewa na tembo, na wengine mashamba yao yameharibiwa,” alisema diwani Kaijage.

Tukio la tembo kuathiri maisha ya binadamu ni la Kijiji cha Rugaze, Kata Kyaitoke baada ya Anajozia Chrisant (43), kupoteza maisha kwa kuvamiwa na tembo kijijini hapo Agosti 6, mwaka jana.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kulia), akizungumza na wajumbe wa Jukwaa la Wafanyabiashara wa Afrika Kusini na Tanzania, wakati wa mkutano wa Jukwaa hilo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## NBC yafungua milango kwa wafanyabiashara

**Na John Badi**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imesisitiza kuhusu utayari wake katika kufanikisha ustawi wa biashara baina ya Tanzania na Afrika Kusini kupitia huduma zake hususani katika eneo la uwekezaji wa biashara na kilimo.

Msimamo huo ulitangazwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Theobald Sabi, alipozungumza kwenye Mkutano wa Jukwaa la Wafanyabiashara wa Afrika uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Sabi alisema kwa muda mrefu sasa benki hiyo imekuwa mdau mkubwa wa wafanyabiashara kati ya Afrika Kusini na Tanzania, akibainisha huduma mbalimbali zinazotolewa na benki hiyo kwa wafanyabiashara hao, zikiwamo huduma za mikopo ya biashara na kilimo.

“Jukumu letu kama benki kubwa nchini ni kuhakikisha tunatoa suluhisho la kibiashara kwa wafanyabiashara wetu ili wafanye shughuli zao kiushindani ndani na nje ya nchi.

“Tumekuwa tukitoa huduma mbalimbali kwao ikiwamo mikopo, bima, uwekezaji amana, kufanya malipo ya aina mbalimbali kati ya nchi, kutuma na kupokea fedha kutoka nje ya nchi.” alibainisha.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wafanyabiashara wa Afrika Kusini, Manish Thakrar, alisema umuhimu wa benki ya NBC na taasisi nyingine za kifedha ni mkubwa hususani katika kipindi hiki ambacho kuna ongezeko kubwa la biashara baina ya Tanzania na Afrika Kusini.

“Tunawashukuru sana NBC tumekuwa nao kwa muda mrefu lakini kwa sasa tunawahitaji zaidi. Changamoto ya COVID-19 pamoja na vita vinavyoendelea baina ya Urusi na Ukraine, vimeongeza sana mahitaji ya bidhaa hususani za vyakula nchini Afrika Kusini.

“Hivyo, kwetu hiyo inaweza kuwa fursa kubwa ikiwa tutachangamkia. Habari njema ni kuwa benki ya NBC imeonyesha kutoa kipaumbele pia kwenye mikopo ya kilimo, hilo litatusaidia sana kwa kuwa bidhaa za vyakula zinahitajika zaidi huko Afrika Kusini,” alisema.

## Visegese wapata uhakika barabara

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

WAKAZI wa Visegese Halmashauri ya Mkuranga, wanatarajia kuondokana na kikwazo cha barabara baada ya kutengwa Sh. milioni 115 kwa ajili ya kufungua barabara hiyo.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini (TARURA), Mhandisi Silas Dilliwa, alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kero ya barabara hiyo inayodaiwa kuwa kikwazo kwa wakulima.

Alisema katika mwaka wa fedha 2022/2023 barabara hiyo imetengewa fedha hizo kwa ajili ya kufungua barabara yenye ukubwa wa kilomita 14.4.

Alisema ukarabati wa barabara ya Nyamaronda Nasibugani yenye urefu wa kilomita 21 unatarajiwa kufanyika kwa muda wa miezi miwili.

Kadhalika, ukarabati wa barabara hiyo utahusisha maeneo korofi, uchongaji wa kilomita 12, kufukia mashimo na kufanya ukarabati kwenye maeneo ambayo hayapitiki kipindi cha mvua.

Barabara hiyo itakarabatiwa kwa gharama ya Sh. milioni 463 na ikikamilika itaondoa usumbufu waliokuwa wakikumbana nao wananchi hususani wakulima wa mazao ya biashara wanaoishi katika maeneo hayo.

Hivi karibuni wakulima wa zao la ufuta pamoja na wasafirishaji walilalamikia kushindwa kufikisha bidhaa hiyo kwenye maghala kwa wakati kutokana na ubovu wa barabara.

Kwa wakazi wa Visegese hii ni mara ya kwanza barabara hiyo kutengewa fedha kwa ajili ya kuifungua na kuleta ahueni ya usafiri kwa wakulima wa korosho, ufuta na nazi.

**Kadhalika, ukarabati wa barabara hiyo utahusisha maeneo korofi, uchongaji wa kilomita 12, kufukia mashimo na kufanya ukarabati kwenye maeneo ambayo hayapitiki kipindi cha mvua.**



## Wapewa jukumu vita ukatili kijinsia

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WADAU wanaojihusisha na kupinga ukatili na udhalilishaji wa kijinsia mkoani Dodoma, wamewahimiza wazazi na walezi kutoa ushirikiano kwa watu na taasisi zinazojishughulisha na masuala ya kupinga vitendo hivyo, ili kupata taarifa na kufanikisha watuhumiwa kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mwezeshaji wa mradi wa kupinga ukatili katika kata ya Mundemu wilayani Bahi, Amos Mlungu kutoka WorldVision Tanzania, alitoa rai hiyo jana alipozungumza na wanakijiji cha Zanka kuhusiana na haki za watoto, hasa elimu.

Mlungu alisema kuwa baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa na tatizo la kutotoa ushirikiano pale wanapohojiwa kuhusu ukatili wa kijinsia unaofanyika katika baadhi ya maeneo nchini na kusababisha watuhumiwa wasipatikane na kuadhibiwa.

"Tunaomba wazazi mtoe ushirikiano pale mnapohitajika kufanya hivyo tunahitaji kuona watoto wanasonga mbele kielimu na siyo kukatisha ndoto zao," alisema Mlungu.

Pia alibainisha kuwa wanafunzi 248 wameshiriki katika uandishi wa insha ya madhara ya mimba za utotoni ili kuwakumbusha kujihadhari na wasirubuniwe na jamii inayowazunguka.

Alisema wanafunzi hao wanashiriki katika kuandika insha hizo kwenye ngazi ya shule, vijiji, kata na tarafa, wilaya na baadaye mkoa kwa lengo la kupata wanafunzi ambao watafanya vizuri.

Aliongeza kuwa ili kuhamasisha watoto kutambua madhara ya mimba za utotoni, wameamua kuandaa mashindano ya uandishi wa insha ili kuwaonyesha kwamba ni wajibu wao kupinga mimba za utotoni.

Shirika hilo pia limetoa mafunzo kwa Kamati za Ulinzi na Usalama katika kata mbalimbali wilayani Bahi na Chemba ili kuimarisha ulinzi na kutokomeza ukatili dhidi ya watoto.

Aliongeza kuwa mafunzo hayo yametolewa katika ngazi ya vijiji, kata, tarafa na wilaya kwa kamati za kutekeleza kutokomeza ukatili dhidi ya mtoto na mwanamke katika maeneo mbalimbali.

Diwani wa Zanka, Deogratius Geuza, aliwataka wazazi na walezi kuwa mstari wa mbele kupinga ukatili wa kijinsia unaofanywa ili kumsaidia mtoto kutimiza ndoto zake.

Alisema serikali inapambana kila kukicha kuhakikisha wanafanikiwa kutokomeza ukatili dhidi ya watoto kwa kuunda kamati mbalimbali za ulinzi na usalama, hivyo wazazi nao wanapaswa kuisaidia.

# Serikali yatenga ruzuku kukabili uhaba mbolea

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIKA jitihada za kusaidia wakulima kupata mbolea, serikali imetenga ruzuku ya pembejeo hiyo ili kuwapunguzia mzigo wakulima na kuvutia wawekezaji zaidi kwenye eneo hilo.

Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, alibainisha hayo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji iliyotembelea kiwanda cha kuzalishaji mbolea cha Itracom kilichoko jijini Dodoma.

Mavunde alisema ruzuku hiyo imetokana na uwekezaji mkubwa wa zaidi ya Sh. bilioni 180 uliofanywa na wawekezaji wa kiwanda hicho kilichoko Nala mkoani hapa.

Alisema serikali imepania kuondoa kero ya mbolea nchini licha ya kwamba iko duniani kote kutokana na bei ya bidhaa hiyo kupanda kwa kiasi kikubwa mara kwa mara.

Pia alisema kwa kuanzia kiwanda hicho cha mbolea kitazalisha tani 600,000 za mbolea kwa mwaka na tani 300,000 za chokaa kwa mwaka ambapo uzalishaji huo utaanza mapema mwezi ujao.

Vilevile, alisema matumaini yao kama serikali na wizara ni kwamba watatibu matatizo ya kudhibiti bei ya mbolea kwa sababu uzalishaji utakuwa unafanyika nchini na wakulima watakuwa wanaipata kwa wakati.

Mavunde alisema moja ya changamoto ambayo inawakabili wakulima ni pembejeo ikiwamo mbolea kuchelewa, lakini kupitia utaratibu huu na kiwanda hicho wanakwenda kutatua shida hizo kwa wakulima.

"Hivi sasa tunakwenda kutatua shida ya mbolea kwa wakulima, serikali itaendelea kuvutia wawekezaji ili kuwapo na pembejeo za kutosha kwa ajili ya wakulima," alisema Mavunde.

Mavunde alifafanua zaidi ya kuwa katika hatua za muda wa kati na mrefu, mojawapo ni serikali kutenga fedha kwa ajili ya ruzuku ya mbolea ili kuwapunguzia mzigo wakulima lakini hatua ya muda mrefu ilikuwa ni kuvutia wawekezaji kuwekeza nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Itracom, Nduwimana Nazaire, aliishukuru Kamati ya Bunge kuwatembelea na kuwatia moyo kama wawekezaji.

Alisema hali hiyo inaonyesha jinsi gani serikali iko pamoja kuhakikisha uwekezaji unakua kwa kiasi kikubwa ili uchumi uendelee kukua nchini.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Dk. Christine Ishengoma, alisema wajumbe wamefurahishwa na uwekezaji unaofanywa huku akiwataka wawekezaji hao kuanza kuzalisha mbolea hiyo kwa muda uliopangwa ili wakulima waanze kuitumia katika msimu ujao wa kilimo.



Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde (wa pili kulia), akiwa pamoja na wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, wakimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda cha uzalishaji mbolea cha Itracom, Nduwimana Nazaire (wa nne kulia) walipotembelea kiwandani hapo, eneo la Nala jijini Dodoma jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

## Wizara yakunwa ujenzi Ofisi ya Msajili Vyama

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu, Kaspar Mmuya, amebainisha kuridhishwa na ujenzi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa katika eneo la Kilimani jijini Dodoma unaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 20.

Mmuya aliyasema hayo baada ya kufanya ziara ya kutembelea ujenzi na kukagua kazi inayofanywa na kampuni ya China ya Group Six International inayosimamiwa na msimamizi kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi.

Akizungumza kwenye ziara hiyo, Mmuya alisisitiza kuongezwa wafanyakazi, muda wa kazi pamoja na vifaa ili kufanya kazi ndani ya kipindi kilichopangwa cha miezi 12.

Alisema kulingana na muda uliowekwa wa ujenzi huo, kuna ulazima wa kuongeza watu na vifaa vya ujenzi ili wakamilishe kwa wakati.

"Hata hivyo, niwapongeze kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa usimamizi mkubwa mnaoufanya lakini endeleeni kuongeza umahiri na kuwasaidia wenzetu wa Group Six ili wafanye kwa matokeo bora zaidi," alisema.

Alimtaka mshauri wa ujenzi kufika mara kwa mara katika eneo la mradi na kufanya kazi kwa kushirikiana na watendaji wengine ili kufahamu hali ya ujenzi na kutatua shida pindi zinapojitokeza.

"Nimshauri mtaalamu wetu awe anatembelea mara kwa mara jengo hili kujionea maendeleo ya kazi, kama kuna shida yoyote inatatuliwa kwa wakati na kufanya marekebisho yanayotakiwa," aliagiza.

Aliwahimiza kuongeza ubunifu wa utendaji kazi kwa kugawa maeneo na muda wa kukamilika kwa kazi kwani itasaidia kuhamasisha kazi kufanyika kwa mwamko na ubora zaidi kama njia ya kuendana na muda wa mkataba unavyotaka.



# Makamu wa Rais awabana makandarasi fedha UVIKO-19

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amewataka makandarasi wote waliopewa miradi ya UVIKO-19 , kutekeleza miradi hiyo kwa wakati kwa kuzingatia viwango na ubora.

Abdulla aliagiza hayo jana wakati akiahirisha kikao cha baraza la wawakilishi na kuagiza Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) kufuatilia kwa karibu miradi hiyo ili kubaini kama kuna ubadhirifu wa fedha hizo.

Abdulla alisema serikali imetenga Sh. bilioni 230 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya UVIKO-19 ambayo imejikita zaidi katika ujenzi wa shule, hospitali za wilaya pamoja na usambazaji wa nishati ya umeme na maji safi na salama Unguja na Pemba.

Alisema utekelezaji wa miradi hiyo ni muhimu utayapatia ufumbuzi matatizo yaliyokuwapo katika sekta hizo muhimu na kuibuwa malalamiko mengi kutoka kwa wananchi ikiwamo kuzorota kwa shughuli za maendeleo.

Aliwataka watendaji, wakiwamo mawaziri na makatibu wakuu, kufuatilia kwa karibu utendaji wa shughuli za miradi hiyo ili kuepuka kasoro zinazoweza kujitokeza mapema na kuchukuwa hatua.

Abdulla aliiagiza ZAECA kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi hiyo ili kuona matumizi halisi ya thamani ya fedha iliyotumika.

Alisema alipata nafasi ya kutembelea baadhi ya miradi ya UVIKO-19 inayotekelezwa na kuridhishwa na utendaji wa kazi zinazofanywa ikiwamo ujenzi wa shule pamoja na hospitali 10 za wilaya Unguja na Pemba.

Kuhusu ujenzi wa masoko likiwamo la Mwanakwerekwe na Bungi ambayo ujenzi wake ulionekana kusuasua na kuwaonya makandarasi waliopewa kazi hiyo kuwa serikali haitasita kusitisha mikataba yao.

“Nimetembelea baadhi ya miradi inayotumia fedha za UVIKO-19 Unguja na Pemba kwa kiasi kikubwa nimeridhika nayo ikiwamo ujenzi wa shule na ukarabati wake pamoja na hospitali 10 za wilaya, lakini sijaridhishwa na kazi za ujenzi wa masoko matatu ya unasuasua sana,”alisema.

Vilevile, Abdulla aliwataka wajumbe wa baraza la wawakilishi kufikisha uamuzi wa Serikali ya Zanzibar ya kukodisha visiwa vidogo kwa wawekezaji kwa ajili ya kukaribisha uwekezaji wenye tija utakaoingiza mapato.

Alisema katika siku za karibuni kumekuwapo na upotoshaji kuhusu matumizi ya visiwa hivyo pamoja na uamuzi wa serikali kuvikodisha visiwa hivyo kwa wawekezaji.

“Wajumbe wa baraza la wawakilishi nendeni kwa wananchi mkafikishe elimu na sababu zilizoifanya serikali kukodisha visiwa vidogo vidogo... uamuzi umefanywa kwa maslahi mapana ya Taifa letu na siyo sababu binafsi za viongozi,”alisema.

Abdulla alisema Serikali ya Zanzibar imewasilisha bajeti ya serikali yenye matumizi ya fedha Sh. trilioni 2.59 ambayo imejikita katika kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kukifungua kisiwa cha Pemba kuwa lango kuu la uchumi na uwekezaji kwa Afrika ya Mashariki na Kati.

Alisema bajeti iliyopitishwa na wawakilishi ni ya kimkakati zaidi ambayo itasimamia na kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2050 katika miundombinu ya uchumi na uwekezaji.



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, akizungumza wakati akifunga kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wizara yaanza utekelezaji wa agizo la Samia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imesema imeanza mchakato wa kujaza nafasi za ajira za walimu 4,000 na kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan ya kuajiri walimu bora wenye viwango watakaotoa ufaulu mzuri kwa wanafunzi.

Waziri wake, Lela Muhamed Mussa, alitoa kauli hiyo jana alipotoa ufafanuzi kuhusu mchakato wa nafasi za ajira za walimu 4,000 zilizotangazwa na Rais Dk. Mwinyi kujaza nafasi za walimu waliostaafu pamoja na shule mpya zinazojengwa kupitia fedha za mkopo wa UVIKO-19.

Mussa alisema jana wakati wa uzinduzi wa Taasisi ya Elimu kwa Wanawake na kusema kuwa suala la ubora wa walimu wanaoajiriwa linatakiwa kuzingatiwa.

Alisema katika ajira hizo mpya, Wizara ya Elimu itazingatia na kupitia ubora wa walimu wakiwamo waliofanya vizuri katika mitihani ya Taifa.

Alisema vigezo vingine ambavyo vitazingatiwa katika ajira mpya za walimu ni mahitaji ya walimu wa masomo ya sayansi ambayo ni moja ya shida kubwa katika shule za sekondari Unguja na Pemba.

“Vigezo vyetu katika ajira mpya 4,000 ni mahitaji ya walimu wa masomo ya sayansi yakiwamo ya Kemia, Baiolojia, Fizikia na Hisabati na ufaulu wake katika mitihani ya Taifa hauridhishi,” lisema.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Ali Abdulgulam Hussein, alisema ajira mpya za walimu zimezingatia mahitaji ya uhaba wa walimu katika shule zilizopo vijijini pamoja na visiwa vidogo vilivyopo Unguja na Pemba.

# Kamishna ajivunia teknolojia ya sensa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMISHNA wa Sensa Zanzibar, Balozi Mohamed Hamza, amesema watatumia vifaa vya teknolojia ya kisasa katika sensa ya watu na makazi ya mwaka huu vitakavyotoa taarifa sahihi.

Mkurugenzi huyo wa Viwango na Uratibu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, alibainisha hayo jana alipozungumza na wahariri na waandishi wa habari kuelezea maendeleo ya maandalizi ya sensa ya watu na makazi.

Balozi Hamza alisema maandalizi ya sensa hiyo yanaendelea vizuri na majaribio yaliyofanywa miezi mitatu iliyopita kwa kiasi kikubwa yameonyesha kuwapo kwa mafanikio.

Aliyataja malengo ya sensa ya watu na makazi ni kuiwezesha serikali kupata taarifa zake muhimu kwa usahihi ambazo zitatumika kwa ajili ya kuleta maendeleo na ukuaji wa uchumi.

“Sensa ya watu na makazi inapofanyika vizuri, maana yake itaharakisha malengo ya serikali katika kupanga matumizi yake kwa ajili ya kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi wake,” alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) Zanzibar, Hassan Khatib, aliwataka waandishi wa habari kuweka mbele maslahi ya Taifa ili kuiwezesha serikali kupata taarifa zake muhimu kwa maendeleo ya Taifa na watu wake.

“Matarajio makubwa ya mafanikio ya sensa ya watu na makazi yapo kwa waandishi wa habari ambao ndiyo watakaofikisha taarifa za umuhimu wa sensa katika kuleta maendeleo ya wananchi,” alisema.

Mwakilishi Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Zanzibar (OCGS), Ali Idrissa, alisema maandalizi ya sensa ya watu na makazi itakalofanyika Agosti 23 yamefikia asilimia 83.

Idrissa aliyataja maandalizi kuwa ni utayarishaji wa ramani zitakazotumiwa na makarani kuhesabu watu katika mitaa na vitongoji.

Alibainisha na kusema ofisi hiyo imejitayarisha kwa nyenzo zitakazotumika kwenye kuhesabiwa ikiwamo vishikwambi (tablets) pamoja na madodoso yatakayojazwa.



GIGY

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI JUNI 25, 2022



# Mara tatu kwani umeroja? Uwoya olewa mwaya

STAA wa filamu, mrembo Irene Uwoya amefunguka kuwa ataolewa hivi karibuni. Tena kasema kabla hata mwaka huu 2022 haujaisha.

Kasema ataolewa kwa sababu yupo kwenye mahusiano mazito na mtu anayependana naye. Ni mahaba shatashata.

Msanii huyo ambaye ni mmoja wa waigizaji wakongwe nchini ameshawahi kuolewa mara mbili.

Mara ya kwanza ilikuwa ni 2007, akiolewa na mchezaji wa zamani wa Rayon Sport ya Rwanda, RSC Anderlecht ya Ubelgiji na hata Stand United ya Tanzania ambayo hakudumu nayo, Mnyarwanda Hamad Ndikumana ambaye alifariki dunia 2017, wakiwa tayari wameshatengana.

Aliolewa na msanii wa hip hop, Dogo Janja, 2017, ndoa ambayo ilidumu kwa miaka miwili tu, wakabwagana.

Hata hivyo mwenyewe amefunguka kuwa kuolewa mara mbili, siyo mwisho wa kumfanya yeye asiolewe tena kwa sababu yote hiyo ni mipango ya Mungu.

"Nitakuja kuolewa hivi karibuni. Mwaka hauwezi kukatika, mwaka huu bado haujaisha msiwe na haraka. Kwanza kuolewa mara moja au mara mbili hakumzuii mtu kuolewa.

Mwanamke ana haki ya kuolewa, hata kama ameacha au ameachika mara elfu 10 au 20. nafasi ya kuolewa ipo pale pale, haijalishi umri wala nini, ndoa ni baraka na Mungu ndiyo anapanga, hakuna binadamu anapanga, kwa hiyo hakuna binadamu anaweza kuzuia hilo," akasema kwa kujiamini.

Uwoya, aliyezaliwa Desemba 19, 1988 ni mwigizaji na mwongozaji wa filamu, mwanamitindo, na mjasiriamali ambaye alipata kushiriki shindano ya Miss Tanzania mwaka 2006, mwaka ambao mshindi wake alikuwa ni mwigizaji, mwanamitindo na mrembo mwenzake, Wema Sepetu.

Alishika nafasi ya tano kwenye kinyang'anyiro hicho akiwa na kina Sarah Kangezi, Jokate Mwegelo ambaye kwa sasa ni mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Temeke na Lisa Jensen.

Ameigiza filamu na tamthilia nyingi, lakini ambayo ilimfanya kuwa staa na kujulikana ndani na nje ya nchi ni 'Oprah'.

**BASI SAWA**

## Wigi la Menina mwisho milioni moja



Msanii Menina Alegria amesema pamoja na kuongezeka kwa tozo la mawigi nchini, ataendelea kununua na kuvaa kwa sababu inaongeza mapato ya nchi, lakini akaongeza kuwa haitozidi la shilingi milioni moja.

Menina ambaye kwa sasa ana ngoma yake mpya iitwayo 'Sijiwezi', anasema kuwa ikizidi tu milioni moja na laki tano, hatonunua.

"Mimi kuongeza tozo hakujanikwaza kwa sababu navaa na kubadilisha fasheni siyo kwa sababu sina nywele, ila ni kwa sababu nimeamua kubadilisha staili tu.

Nywele zangu hapa ni wigi tosha, ukinivua hapa wigi utakutana na lingine, ni vizuri serikali kupandisha tozo kwa sababu ni kuongeza mapato kwenye nchi yetu. Ila ni kwa sababu nimeamua kubadilisha staili tu.

Nitaendelea kununua na kuvaa. Bei yangu ya mwisho ni shilingi milioni moja, ikifika milioni moja na laki tano sinunui, mwisho wangu ni milioni moja.

Mimi niwashauri wanawake wenzangu watunze nywele zao ili hata mawigi, yasipokuwepo kabisa wawe na cha kujivunia."

## Lon Bway mashine tatu

Msanii wa muziki wa kizazi kipya Lony Bway, ametangaza ujio wa EP yake iitwayo 'Mashine Tatu' ambayo ameachia rasmi jana.

Kupitia mtandao wake wa kijamii, akaandika " Rasmi kabisa hii ndiyo EP kava yetu, Mashine Tatu, inayotoka Ijumaa." Alitoa taarifa hizo.

Msanii huyo anayekuja kwa kasi, ameshatoa ngoma kibao kama 'Sinyorita', 'Nawewe', 'Nimeshindwa', 'Tunalala' na nyingine nyingi.



## He, Gigy, milioni 32 birthday tu?

Msanii Gigy Money ameweka wazi kuwa alitumia Sh. Milioni 32 usiku mmoja kwenye sherehe ya kuzaliwa kwake 'birthday'.

Kwenye pati yake ya kutimiza umri wa miaka 25, msanii huyo alisema aligharamia kila kitu kwenye usiku huo kuanzia vyakula, vinywaji na ukumbi na alikaa na mastaa kadhaa kama Wema Sepetu, Mimi Mars, Lulu Diva, Amber Lulu na Baba Levo.

"Milioni 32 zilinitoka kwenye siku yangu ya kuzaliwa, nchi zingine wanaichukulia kwa umakini sana siku hii ya kuzaliwa, sisi tu hapa tunaichukulia poa. Teketeza chochote, umezaliwa siku moja na utakufa siku moja, bongo ndiyo tunaichukulia poa, nchi kama Nigeria, Marekani wanaichukulia kwa umuhimu sana."

## Baba Mkwe: Mzazi mpenda pesa kama mfuko

**Na Adam Fungamwango**

NI filamu inayowaonya wazazi wanaopenda kuwachagulia watoto zao wachumba.

Ikumbukwe kuwa kuoa au kuolewa, unategemea kuishi na mtu huyo maisha yako yote.

Hivyo kitendo cha kumchagulia mtu wa kuishi naye si cha kiungwana.

Binadamu kwa kawaida hupenda kuishi au kuwa karibu na mtu anayempenda kutoka moyoni mwake.

Hata kama akiwa na kasoro gani. Mtu yoyote ambaye hajai kwenye moyo wa mtu, hawezi kuishi naye.

Na hata kama akilazimishwa ataishi naye kwa muda mfupi tu.

'Baba Mkwe' ni filamu inayomuonyesha mzee Jengua ni baba mwenye tamaa, anayependa pesa, hivyo anamchagulia binti yake Mioyo mwanaume wa kumuoa.

Imechezwa na Flora Mvungi, Mzee Jengua mwenyewe, Mzee Msisiri, Tatu Mnaly na wengineo.

Mioyo anamwambia mama yake kuwa amepata mchumba ambaye ni Kazembe. Ni mtoto wa marehemu mzee Jongo. Hata hivyo jambo hilo linapingwa na mzee Jengua kwa sababu ni masikini.

Kwenye kijiji hicho, mtoto wa mzee Msisiri aitwaye Rama anawasili baada ya kumaliza elimu yake ya chuo huko mjini.

Baba yake anamwambia aoe. Yeye na mzee Jengua wanapanga kuwaozesha Rama na Mioyo.

Barua ya posa inapelekwa, mzee Jengua anaipokea kwa sababu Rama ni msomi na pia ukoo wake unajiweza.

Binti anakataa kata kata, akisaidiwa na mama yake. Kitendo hicho kinamfanya mzee Jengua kuwa mbogo na kuwapa adhabu wote wawili binti na mama yake.

Kazembe naye akajaribu kupeleka posa nyumbani kwa kina Mioyo, lakini akaishia kudhalilishwa na kutimuliwa kwa panga mkononi.

Binti akaamua kutoroka nyumbani.



Haikuwa dawa, kwani alitafutwa na baada ya kupatikana akarudishwa nyumbani, mpango mkakati ukawa ni ule ule wa kumuoza kwa Rama na si Kazembe.

Wakati sherehe za harusi zikiandaliwa kati ya Rama na Mioyo, Kazembe anachukua uamuzi ya kujinyonga.

Ilikuwa ni huzuni na vilio kijijini hapo, lakini kwa mzee Jengua yeye kwake ikawa ni nderemo na vicheko.

Mtu aliyekuwa akimzuzua binti yake amekwenda. Siku ya harusi imefika, bwana harusi anamsubiri bibi ili ndoa ifungwe.

Bi. harusi wakati anatoka chumbani, hatua ya kwanza, ya pili ya tatu, akaanguka povu likamtoka mdomoni. Akafariki dunia. Kumbe alikuwa tayari amekunywa sumu ili asiolewe na mtu asiyempenda, huku aliyempenda tayari akiwa marehemu. Sherehe za harusi zinageuka msiba.



## Harmonize, Kajala mambo hadharani

Baada ya muda mrefu wa kutafutana huku na kule, hatimaye msanii wa bongo fleva, Harmonize na Kajala ni kama vile tayari wamesharudiana.

Kupitia akaunti zao za kijamii wawili hao wameonekana kila mmoja kuposti picha zinazoonyesha kuwa penzi limerejea.

Wapenzi hao ambao huko nyuma walishawahi kuwa pamoja wakazinguana, wameonekana kuwa pamoja na kufuahia tena penzi lao.

Ingawa hakuna yoyote aliyetamka kwa kinywa chake, lakini picha zao zinaongea.

Harmonize yeye kwenye mtandao wake wa kijamii ameamua kuposti picha kadhaa akiwa na mwigizaji huyo wa zamani, lakini yeye Kajala ameposti video fupi wakiwa kwenye ukumbi wa mazoezi 'gym'.

Kufuatia picha hizo za mnato na video kwa hao wote wawili, msanii na mwigizaji Aunt Ezekiel, yeye kaandika kwenye mtandao wake wa kijamii "Hatimaye"

## MICHANGO YA HARUSI IMEFANYIWA BIASHARA

**Na Adam Fungamwango**

WASANII nao wana mambo kweli kweli. Ukiwafuatilia kwenye mitandao yao ya kijamii, unaweza kukauka sauti kwa kucheka au kuumia mbavu.

Unajua wasanii wote, wawe wa bongo fleva, filamu, tamthilia, hip hop, au hata wanamuziki, pamoja na kuburudisha watu wana maisha yao ya kawaida kama binadamu wengine.

Nao wanaungana na jamii kushea mambo mbalimbali kwenye mitandao ya kijamii, ikiwa ni lengo ya kuburudika, kuelimika na kuelimisha.

Nimetembelea kwenye mtandao wa kijamii wa instagram na kukutana na posti nyingi, lakini leo nimeamua kuziweka hizi ambazo baadhi ya wasanii wameziweka kwenye mitandao yao ya kijamii.

**Peter Msechu**

Huyu ni msanii mwimbaji ambaye ukiingia kwenye mtandao wake wa kijamii, kama hukucheka basi utakuwa na matatizo. Yeye posti zake nyingi ni za ucheshi, hata kama ni za kuelemisha au za kufundisha, lakini ataziweka kwenye hali ya ucheshi, kiasi cha kueleweka kirahisi. Yeye kaandika hivi.

"Kama ulinichangia mchango wako kwenye harusi yangu basi kaa ukijua ulinipa mtaji mkubwa wa kibiashara. Pole sana Kajala hiki ndicho nilichofanyia."

**Jacob Steven JB**

Ni mmoja kati ya mastaa nguli wa filamu na tamthilia. Kwenye mtandao wake wa kijamii aliandika maneno haya "Moja kati ya tatizo kubwa tulilo nalo kwenye tasnia yetu ni waigizaji kujirudia.Unakuta mwigizaji mmoja anacheza tamthilia nne kwa pamoja, kuna haja ya kuleta waigizaji wapya."

**Irene Uwoya**

Mwigizaji filamu na tamhilia, mwanamitindo na mjasiriamali, Irene Uwoya yeye wala hakuwa na maneno mengi kwenye mtandao wake wa kijamii. Akaamua kuposti maneno yanayosomeka kama ifuatavyo.

"Hivi ni kweli bahari haipimwi kwa mguu?" Mmh, hapa sijui alitaka jibu gani. mbona linaeleweka tu?

**Jenifer Kyaka 'Odama'**

Alianza kujulikana kwenye filamu ya Shumileta na Beyonce. Mwigizaji huyu ambaye kila miaka inavyozidi kwenda anazidi kuwa mrembo, yeye kwenye mtandao wake wa instagram kaandika maneno haya.

"Tambua kuwa kila siku ni zawadi , hakuna heshima inayozidi uhai. Tuseme ahsante Mungu kwa siku mpya..."

**Vicent Kigosi 'Ray'**

Ni mmoja wa waasisi wa tamhilia na filamu nchini Tanzania ambaye bado mpaka sasa ameendelea kuwa juu kwenye tasnia hiyo. Kuna maneno ameyaandika kwenye mtandao wake wa instagram.

"Kuna muda neno hisia huwa ni ngumu kulificha kutokana na maumivu makali ndani ya mioyo yetu na ndipo sisi binadamu huwa tunaamua kuweka wazi hisia zetu kwa tunaowapenda."



# Davido afanya kufuru kwa mtoto wake



MWANAMUZIKI David Adeleke, maarufu kama Davido, ameonyesha nguvu yake ya kifedha baada ya kumzawadia mtoto wake wa kiume, Ifeanyi, saa ya mkononi yenye gharama kubwa.

Mkali huyo wa muziki ambaye ni bilionea alimpatia mtoto wake huyo wa miaka miwili saa aina ya Audemars Piguet, ambayo ina gharama ya kiasi cha naira milioni 150 sawa na dola 350,000.

Hii itakuwa mara yake ya kwanza kutumia kiasi kikubwa cha fedha kununua saa kwa ajili ya mtoto, lakini kwa upande wake amekuwa kama kichaa wa bidhaa hiyo kwani kila wakati anatumia pesa nyingi kununua matoleo mapya.



## Mercy hapo unaenzi ya Mungu

MWANAMUZIKI wa Injili wa Nigeria, Mercy Chinwo, hatimaye ametangaza kuwa na mwenza baada ya kuvishwa pete ya uchumba .

Staa huyo ametumia ukurasa wake wa Instagram akiandika jinsi anavyojiona kubarikiwa na Mungu kumpata mwanaume ambaye ataishi naye daima.

"Nabariki katika kubarikiwa na Mungu kwa kumpata mwanaume mwenye unyenyekevu na heshima kwangu," ameandika Mercy.

## Portable bado unahitajika polisi

MSANII wa muziki mwenye utata mwingi nchini Nigeria, Portable, ametangaza kufunga ndoa na mama wa mtoto wake, siku chache baada ya polisi kumtaka ajisalimishe kutokana na tukio la kikatili.

Hivi karibuni mwanamuziki huyo alitakiwa kujisalimisha kituo cha polisi baada ya video iliyosambaa mitandaoni ikimuonyesha akiwaamuru walinzi wake kumpiga kijana mmoja.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Portable, hakuonyesha kujutia tukio hilo, badala yake aliandika jinsi anavyojisikia furaha kumpata mtoto wa kike na kisha kutangaza kumuoa mwanamke huyo.





## Burna Boy kupoteza mwelekeo?

MKALI wa muziki wa Afri Pop, Burna Boy, huenda umaarufu wake ukaporomoka kutokana na kuandamwa na matukio mengi ya ukatili.

Katika tukio la hivi karibuni, mwanamuziki huyo na rafiki zake inadaiwa walivamia klabu moja ya usiku na kutembeza kipigo kilichowaacha watu kadhaa wamejeruhiwa.

Tukio kama hilo alilifanya miaka miwili iliyopita baada ya kuvamia klabu moja ambayo Davido alikuwa akitumbuiza na kuzusha vurugu.

Katika tukio hilo, wasanii hao wawili waliishia kupigana na kuibua malalamiko kuwa Burna Boy alihusika kuanzisha vurugu hizo kutokana na kuvamia klabu hiyo bila kutoa taarifa

## Chappelle ashambuliwa jukwaani

MSANII wa ucheshi kutoka Marekani Dave Chappelle, amepata tukio la kushtushwa baada ya kuvamiwa na mtu mmoja mwenye kisu wakati yupo jukwaani akiburudisha.

Kulingana na taarifa mbalimbali, tukio hilo lilitokea katika ukumbi maarufu wa Hollywood Bowl, mbele ya watu waliokuwa wakihudhuria tamasha lake.

Mshambuliaji huyo huyo alikuwa na kisu chenye umbo la bunduki, lakini alikamatwa.

Katika video ambayo imesambaa mitandaoni inaonyesha mtu huyo akimuangusha chini Chappelle na alijaribu kukimbia nje ya jukwaa kabla hajakamatwa na wana usalama.



# Msalaba Mwekundu Tanzania inavyookoa jamii ya kifugaji kukabiliana na ukame

Na Mwandishi Wetu

UKAME ambao umekuwa ukizikumba baadhi ya wilaya za mikoa ya Arusha na Manyara, umezifanya jamii zinazoishi maeneo hayo kukabiliana na changamoto nyingi ikiwamo ukosefu wa chakula na mifugo kufa.

Tatizo la ukame linalojitokeza mara kwa mara hupelekea kuongezeka kwa watoto wanaokumbwa na utapiamlo, kurudi nyuma kiuchumi kutokana na mifugo kufa kwa kukosa malisho na maji na nyasi.

Hata hivyo, kumekuwapo na jitihada zinazofanywa na wadau mbalimbali wanaoshirikiana na serikali kunusuru wakazi wa maeneo hayo wanayoishi jamii ya wafugaji ili kusaidia watoto kuepuka tatizo la utapiamlo.

Miongoni mwa wadau hao ni Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania (TRCS), ambacho kimekuwa kikifika kutoa msaada wa kibinadamu kwa waathiriwa wa ukame katika wilaya za Monduli na Longido mkoani Arusha.

Pia inashiriki kikamilifu katika wilaya za Mbulu na Simanjiro mkoani Manyara.

Katika mkakati huo taasisi hiyo inatoa msaada wa chakula, matunda, dawa na fedha taslim, ili kupoza machungu yaliyotokana na ukame.



Mmoja wa wanufaika wa ungalishe uliotolewa na Chama cha Msalaba Mwekundu, akipika uji. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

### MSAADA ULIOTOLEWA

Mkurugenzi wa maafa wa chama hicho Tanzania, Robi Wambura, anasema tangu Februari mwaka huu walianza kutoa huduma mbalimbali za kijamii katika maeneo hayo na kwamba Aprili mwaka huu walirudi tena kutoa msaada wa fedha na vyakula.

Anafafanua kuwa msaada wa kifedha wenye gharama ya shilingi milioni 98, umezinufaisha kaya 700 katika wilaya za Longido mkoani Arusha, Simanjiro na Mbulu mkoani Manyara kila moja ilipata 140,000.

"Wiki iliyopita, tulirudi tena na kutoa msaada wa fedha, vyakula, matunda na dawa katika wilaya za Mbulu, Simanjiro, Longido na Monduli," anasema Wambura.

Anafafanua kuwa katika utoaji wa msaada kwa awamu ya tatu kaya 1200 zilinufaika kwa kupewa kiasi hicho cha fedha. Kaya nyingine 150 zilipewa ungalishe, matunda na dawa, na kufundishwa jinsi ya kupika uji.

"Tutaendelea kuwa na jamii hiyo wakati wa maafa na hata wa raha, hivyo nao waendelee na imani na sisi wawe karibu katika kusaidiana pale inapohitajika," anasema Wambura.

Wambura anaeleza kwamba mwezi Julai chama hicho kitarudi katika wilaya hizo, kwa ajili ya kuendelea kutoa msaada ikiwa ni mwendelezo wa kusaidia waathiriwa wa ukame.



Mkurugenzi wa maafa wa chama hicho, Robi Wambura (kushoto), akimsaidia mmoja wa waathiriwa wa ukame wilayani Mbulu, kupokea msaada wa fedha zilizotolewa na chama hicho. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

"Tunafanya kila njia kunusuru jamii hizi, hasa watoto wasikumbwe na ugonjwa wa utapiamlo, hivyo tuendelee kushirikiana kwa kila mmoja kutoa chochote alichonacho," anasisitiza.

Anaongeza kwamba majukumu yao wanasimamia na kuzingatia kanuni zao saba ambazo ni ubinadamu, uadilifu, kutopendelea, uhuru, kujitolea, umoja na ulimwengu.

Mkurugenzi huyo wa maafa anasema, chama hicho kinawezeshwa na Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Msalaba Mwekundu (IFRC), kufanya kazi ya kutoa huduma mbalimbali za kijamii.

Mwezi ujao wa Julai tutarudi tena kwenye wilaya hizo, na kwamba wanaendelea na maandalizi yatakayowawezesha kufanikisha kile walichokikusudia kwa waathiriwa wa ukame.

Aidha, anasema, chama hicho kilishiriki kikamilifu kwenye janga la corona kwa kwenda katika jamii na kuielimisha kuhusu madhara ya janga hilo na kuhakikisha inachukua tahadhari zote zinazotakiwa.

"Chama cha Msalaba Mwekundu ni kisaidizi cha serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, hivyo tulishiriki kikamilifu kutoa elimu kwa jamii na kufuatilia ili kujua ni jinsi gani jamii inavyozungumzia corona," anasema.

### MSAADA UTUMIKE VIZURI

Kaimu Ofisa Maafa wa Wilaya ya Longido, Albert Israel, anawataka wale wote waliopata msaada kutoka TRCS, kuutumia kama ulivyokusudiwa ili kukuza ustawi wa familia zao.

Anasema, inawezekana wakadhani kwamba msaada wa aina hiyo unaweza kuwa unatolewa kwao tu na kusahau kuwa Tanzania ni kubwa na kwamba yapo maeneo mengine ambayo TRCS inatoa huduma.

"Tunawashukuru Msalaba Mwekundu kwa msaada wenu na jinsi mnavyoonesha kujali waathiriwa hawa wa ukame, lakini pia ni muhimu mliopata msaada mkautumia kujikimu na siyo mambo mengine," anasema Israel.

Naye Meneja Maafa wa TRCS Samuel Katamba, anafafanua kuwa chama hicho kinatoa huduma mbalimbali katika jamii pale majanga mbalimbali yanapotokea yakiwamo yanayosababishwa na vita, magonjwa na maafa ya asili.

"Jambo la msingi ni kwamba tunaomba ushirikiano wenu tunapotimiza majukumu yetu katika jamii, hivyo ni kwamba tupo pamoja katika shida na raha tuendelee kushirikiana," anasema Katamba.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Kutoka jiko la stovu hadi la gesi

## •jiko la mchina mkombozi wa mabachela

Na Adam Fungamwango

SIKU hizi unapofika nyumbani, unaandaliwa au kuandaa chakula asilimia kubwa ya watu hutumia majiko ya kisasa.

Anayetaka kupasha moto chakula au mboga, atatumia kitu kimoja kinaitwa 'microwave oven'. Anayetaka kuandaa chakula atatumia jiko cha umeme, siku hizi pia kuna jiko la gesi.

Haya yote ni majiko ya kisasa ambayo yamekuja kuleta mapinduzi makubwa kwenye masuala ya vyombo vya jikoni.

Majiko yote haya yanaivisha chakula upesi na hawa watu hawasubiri chakula kwa muda mrefu kama zamani.

Utakumbuka zamani, miaka ya 1990 kurudi nyuma wakati wanafunzi wanaporejea majumbani mwao, wanapofika wakati mwingine wanakuta ndiyo kwanza mboga inapikwa.

Kwa bahati mbaya mboga yenyewe iwe maharage, ndiyo utakoma ubishi. Na kwa bahati mbaya zaidi, baadhi ya maharage ya zamani yalikuwa hayaivi upesi, wakati mwingine hadi kwa magadi.

Na inawezekana kabisa mwanafunzi ukafika nyumbani, badala ya kupumzika ukaambiwa ukatafute kuni za kuongezea pale kwenye mafiga ili maharage yaive upesi.

Kama wakati ule kungekuwa na majiko kama haya, wala watoto na wanafunzi wasingeteseka kusubiri kwa muda mrefu, au kuambiwa wakaokote kuni, au vifuu kwa wale walioishi mikoa ya Pwani ikiwemo Dar es Salaam.

Ndiyo yalikuwa maisha ya enzi hizo. Kulikuwa na aina kama nne ya majiko, ambayo kwa kiasi kikubwa ndiyo yaliyotumika kwa mapishi.

### JIKO LA KUNI

Halikutumika vijijini tu, bali hata kwenye majiji makubwa hususan Dar es Salaam. Wale ambao hawakutumia mafiga na kuni kwenye miji mkubwa ni wale ambao uwezo wao ulikuwa mkubwa. Labda wale waliokuwa wafanyabishara wakubwa, wenye nyadhifa serikalini, na wengine wanaofanana na hao.

Lakini familia za kawaida hata Dar es Salaam enzi hizo zilitumia kuni kwenye kutayarisha chakula.

Inawezekana wakawa na aina nyingine ya majiko, lakini hii haikutumia gharama kubwa sana, zaidi ya kuokota au kwenda kununua kuni.

Vijijini suala ya kutumia kuni ni la kawaida hadi leo hii, ingawa na wao pia wanaanza kuondoka huko taratibu.

Aina hii ya jiko ni kwamba mawe matatu yanapangwa, lakini katikati zinawekwa kuni na kuwashwa. Yale mawe matatu hutumika kuwekea chungu au sufuria ili kupikwa kitu kinachotakiwa kipikwe.

Wakati vijijini kuni zinaokotwa porini, kwenye miji mikubwa Dar es Salaam wakati huo nayo pia baadhi ya maeneo yalikuwa mapori, hivyo kuni zilipatikana kwa wingi.

Halafu pia kulikuwa na vifuu vya nazi vilivyo kauka, pamoja na makumbi yake, ambayo nayo yalitumika kama kuni.

Dar ni Dar tu, yale maeneo ambayo yalikuwa katikati ya mji ambayo hayakuwa na mapori sana kulikuwa na maeneo ambayo walikuwa wanauza kuni. Yaliitwa lingo.

"Nenda kaninunulie kuni lingoni." Mtu ataagizwa.

Hata sasa ukienda maeneo ya Temeke na Tandika, bado unaweza kuona maeneo ambayo zamani yalikuwa ni malingo ya kuni, yaani maeneo ambayo kuni zilikuwa zinauzwa.

Sehemu yoyote ambayo kuni ziauzwa ni lazima kwanza uzungishiwe miti, halafu katikati yake ndiyo kuna kuni za aina mbalimbali, pamoja na miti mingine ambayo ilikuwa ikitumika kujengea nyumba za udongo wakati huo.

### JIKO LA MKAA

Haya ni majiko maarufu sana Dar es Salaam na mikoa mingine, hasa ya Pwani. Mikoani kwa asilimia kubwa walikuwa wanapikia kuni, lakini mkaa ulikuwa unatumika sana kwenye miji mikubwa ambayo iliitwa ya mjini.

Aina hii haihitaji kupuliza ili iwake kama kuni, bali mkaa ukishakolea basi wenyewe unawaka moja kwa moja.

Jiko la mkaa linahitaji mkaa ambao ni miti iliyochomwa.

Hii ni aina ya pili ya majiko yaliyotumika sana enzi hizo, ingawa kwa sasa kutokana na serikali kuanza kupiga marufuku matumizi makubwa ya mkaa, kutokana na kuchoma hovyo miti, imepungua.



Enzi hizo, ukiondoa jiko la kuni lililoonekana ndiyo la hali ya chini kabisa, basi juu yake linakuja jiko la mkaa.

Kama ilivyo jiko la kuni, aina hii ya majiko mara nyingi hupikiwa vyakula ambavyo vinachukua muda mrefu kuiva kama vile maharage, njugu mawe, kande na vingine vinavyofanana na hivyo.

Halafu pia akinamama wa Pwani, hupenda majiko haya kwa sababu ya kupikia wali. Ni kwa sababu staili yao ya mapishi wakishamaliza kupika kuchukua mikaa kadhaa ya moto na kuiweka juu ya mfuniko uliofunikiwa sufuria ya wali. Hapa unapata kitu kinaitwa matandu anapopakua chakula hicho.

Aina hii ya mapishi huwezi kuipata ukipika kwenye jiko lolote la kisasa hadi hii leo. Ndiyo maana wapo akinamama mpaka leo wana majiko ya mkaa ambayo yanatumika kupikia vyakula ambavyo wao wanaona havina ladha nzuri vikipikwa kwenye majiko ya kisasa.

### JIKO LA MCHINA

Linaitwa hivyo kwa sababu litengenezwa na Wachina enzi hizo. Ni aina ya majiko ambayo yalikuwa yakitumiwa zaidi na wanaume ambao hawajaoa. Ni kwa sababu ilikuwa si rahisi kwao kutumia majiko ya kuni na kuanza kupuliza, au kwenda stoo kununua mkaa. Kwa wanaume kwao waliona aibu.

Jiko la Mchina likawa ndiyo mkombozi. Mtu anatoka kwenye mishughuliko yake, anawasha jiko na kupika ugali au wali, huku mboga yao kubwa ni maharage ya kwenye kopo, samaki wa kukaanga au nyama ya kwenye kopo, maarufu kama 'bifu'.

Unachotakiwa kufanya kwenye aina hii ya jiko ni kununua mafuta ya taa tu na kuyamimina kwenye chombo chake kilicho chini kinachoonekana kama bakuli kubwa hivi, halafu kunakuwa na tambi, zilizoitwa tambi za jiko.

Kila kitu kikiwa tayari unawasha tambi hizo ambazo zina kitufu chake cha kupunguza na kuzidisha, unaweka sufuria juu, kazi ya kupika inaanza.

Tatizo ni kwamba moshi mwembamba wa jiko hilo unawasha sana machoni na hasa jiko hilo linapokuwa limezimwa.

Wakati likiwa jipya, unaweza kuzima kwa kitufe tu, lakini likishaanza kuwa kuukuu ni lazima uzime kwa kutumia maji kidogo ambayo unayaweka kwenye kiganja na kuyarusha kwa nguvu katika jiko hilo. Kama halikuzimika utarudia tena hadi lengo litimie.

Akinamama waliyatumia, lakini sijui kwa nini hawakuwa wanayapenda sana majiko haya. Waliyatumia mara nyingi kama kuchemshia mboga, au kupikia ugali tu nyakati za mchana kwa sababu ya kutaka kufanya haraka, lakini kama wanataka hasa wakae na kupika, walitumia zaidi ya mkaa kuliko majiko haya ya 'mabachela'.



### JIKO LA STOVU

Ndiyo majiko ya gharama na ya hali ya juu kwa wakati huo. Yalitwa majiko ya stovu. Si kila mtu alikuwa nayo.

Unaweza kusema ndiyo majiko ya gesi ya wakati huo, kwa sababu jinsi yalivyokuwa yakiwaka ule moto wake, na hata muonekano ni kama haya ya gesi kwa sasa ambayo mengi tunayaona majumbani.

Yaliivisha chakula au chochote kinachopikwa haraka zaidi kuliko aina zote hizo za majiko.

Kwa sasa hayaonekani au hayapo kabisa. Lakini unapoyaona majiko ya gesi yenye mitungi midogo, moto wake wa bluu na hata sauti yake wakati unawaka ni vile vile kama stovu.

Utofauti upo kwenye kuwasha tu. Jiko la gesi unazungusha kitu kama kigurudumu ili kuruhusu gesi kupanda, halafu unawasha kiberiti moto unawaka.

Stovu au jiko la gesi ya zamani yenyewe unapitia mchakato kadhaa. Kwanza unahakikisha tanki lake la chini lina mafuta ya kutosha.

Unaanza kupampu kitufe chake kupeleka mbele na nyuma, hadi mafuta yanaanza kuruka kupitia kitundu kidogo juu na kulowesha sehemu iliyowekwa maalum kwa ajili ya kuwashia moto.

Moto unapowashwa, utawaka kwa dakika kadhaa kwenye chombo hicho kilichotengwa, mpaka unapokaribia kuzimika, ndipo mtumiaji atakapoanza kupampu tena kile kitufe cha kwanza. Safari hii mafuta hayatoki tena, bali ni moto wa bluu pamoja na sauti kama ile inayolia kwenye moto wa gesi ndiyo itachukua nafasi yake.

Hapo tayari kazi ya kuwasha imekamilika, kinachofuatia ni kupika tu.

Awali majiko haya yalitoka nchini Sweden na kuwa maarufu sana nchini, lakini baadaye yalianza kutoka matoleo mengine kutoka kwenye nchi zingine ambayo hayakuwa na ubora kama wa mwanzo, ndipo umaarufu wake ulipoanza kupungua na baadaye kutoweka kabisa.

**Tuma meseji 0716 350534**

## Watendaji waonywa hujuma katika ugawaji wa pembejeo

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali, Marco Gaguti, amewaonya watendaji wa serikali pamoja na madiwani mkoani humo kutojihusisha na vitendo vya kuhujumu ugawaji wa pembejeo za kilimo cha korosho zinazoendelea kugawiwa kwa wakulima.

Aidha, amesema serikali itamfikisha kwenye vyombo vya sheria mtu yeyote atakayekamatwa akihujumu pembejeo hizo.

Alitoa agizo hilo jana katika kikao maalumu cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Masasi kilichokaa kwa ajili ya kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali( CAG) kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri hiyo.

Gaguti alisema hadi sasa kiasi cha pembejeo za kilimo zaidi ya kilo milioni mbili tayari zimegawiwa kwa wakulima wa korosho mkoani humo.

"Natoa onyo kali kwa mtendaji yeyote au diwani kujihusisha kuhujumu zoezi la pembejeo za kilimo tutachukua hatua dhidi yake sisi ndiyo tunatakiwa kuhamasisha na kusimamia vyema ugawaji wa pembejeo hizo," alisema Gauguti

Alisema malengo ya serikali ni kuona kila mkulima mwenye sifa na vigezo anapatiwa pembejeo za kilimo na pembejeo zilizo sahihi kwa matumizi ya zao hilo.

Aidha, alisema wako baadhi ya watendaji wa serikali na madiwani ambao walijaribu kuhujumu kwa kutoa pembejeo feki kwa wakulima na tayari serikali imeshachukua hatua dhidi yao.

Alisema wakulima wanaendelea kupata pembejeo kwa utulivu katika maeneo yao na kwamba wakulima wataongeza tija ya uzalishaji wa zao la korosho katika mkoa Mtwara.

Katika hatua nyingine Gaguti amezipongeza Halmashauri zote tisa kwa kuweza kupata hati safi za mahesabu kwa mwaka wa fedha, 2021/ 20222 .

# Makalla atoa miezi 2 kurudishwa bilioni 10/-

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amewataka makandarasi wa taka, wakala wa ukusanyaji mapato na watumishi 19 wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, waliofanya ubadhirifu wa zaidi ya Sh. bilioni 10 kuzirudisha ndani ya miezi miwili.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani, Makalla alisisitiza endapo wahusika waliofanya ubadhirifu wa fedha hizo hawatarudisha ndani ya muda alioutoa atawakabidhi kwa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa nchini (TAKUKURU).

Pia alitoa siku saba kwa Mkurugenzi wa Jiji, mkaguzi wa ndani, msimamizi wa mfumo wa mapato na mhasibu, kuhakikisha wanatoa maelezo ya kina ya maandishi kujieleza kwa nini wameshindwa kudhibiti ubadhirifu wa fedha hizo.

"Baada ya wahusika hao kuhojiwa, baraza la madiwani liliketi na kupitia upya kasoro zote zilizoonekana na kuhakikisha mnatoka na maazimio ya kuzitatua," alisisitiza Makalla.

Vile vile, alisema hatua hiyo imekuja baada ya ukaguzi maalumu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2020/2021 kuonyesha Sh. bilioni 10 zilikusanywa, lakini hazionekani kwenye mfumo.

Alibainisha kuwa kwa mujibu wa ripoti ya CAG, mawakala hawajawasilisha Sh. bilioni 4.4 na watumishi hawajaweka kwenye mfumo wa fedha zaidi ya Sh. bilioni 5.4 ambapo mpaka sasa hakuna aliyechukuliwa hatua licha ya CAG kuagiza fedha hizo kurejeshwa.

Alitaja watumishi hao kwa majina na fedha walizozifanyia ubadhirifu katika mabano akiwamo Jeska Jonathan, Sh. milioni 712, Nissa Mwakasia (milioni 494), Juma Omari (milioni 484), Deogratius Benedikto (bilioni 1.9), Josephine Sandewa (milioni 668), Kiala Shabani (milioni 79), Muongozi Chingile (milioni 24).

Wengine ni Faraja Kalaze (milioni 93), Pius Majura (milioni 96), Felix Balema (milioni 42), Elinaswe Abeli (milioni 56), Msombola Saidi (milioni 31), Sofia Nkusa (milioni 31), Omari Mwesongo (milioni nne), John Mfugale (459,000), Majura Mutalemwa (milioni 39), Tatu Mkangwa (milioni 77), FelishianiMarro(milioni460)na Rostati Tibaijuka (milioni tano).

"Madiwani mmepewa dhamana kubwa nyie ni jicho kwa niaba ya wananchi, timizeni wajibu wenu ilindeni halmashauri yenu, fedha hizi tunatakiwa kujua ukweli ziko wapi, haikupaswa mkurugenzi na mkaguzi wa ndani kuwapa madiwani taarifa, kila mmoja anahaki ya kujua hii taarifa yote."

"Wanaotajwa watoke waje kwenye kamati ya fedha, madiwani muamue hapa, hakuna kupitisha kitu msichokielewa, mawakala na kila mmoja alivyotajwa ndani ya siku 60 warejeshe fedha zilizotajwa, hatua ya pili baada ya muda huo nitawakabidhi wote TAKUKURU kwa ajili ya kufunguliwa kesi," alisema Makalla.

Alisema kutokana na uwapo wa miamala inayosomeka kama ni mapato, lakini kutokuwa na uhalisia, aliwataka kila mmoja kueleza kiasi halisi anachodaiwa na wasiporidhika nayo watawapeleka mahakamani.

Makalla alielekeza mabaraza ya madiwani katika halmashauri zote za mkoa huo kutimiza wajibu wao ikiwa ni pamoja na kujiridhisha kwa kina na kila taarifa wanazopitisha kwenye vikao vyao kuwa ni sahihi.

Vilevile, alielekeza halmashauri hiyo kufanyia kazi hoja 18 zilizobaki kati ya 49 zilizotolewa na CAG katika ripoti yake na kuhakikisha zinafungwa na kutojirudia.



Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari wa Vodacom Tanzania Plc, Athuman Mlinga (katikati), akiwasilisha mada kwenye mdahalo kuhusu utawala na uhakika wa TEHAMA, wakati wa mkutano wa mwaka wa ISACA Tanzania, jijini Arusha juzi, ambapo wataalam wa masuala ya usalama wa mtandao na teknolojia walikutana kujadili namna ambavyo kila mmoja anaweza kushiriki katika kuimarisha usalama wa mifumo yake. Kushoto ni Mkaguzi Mkuu wa hesabu za ndani wa TASAC, Ahadi Chacha na Mshauri wa Teknolojia ya Habari wa KPMG, James Chotamawe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC asaka walioshindwa kurejesha mikopo

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MKUU wa Wilaya ya Bukoba, Moses Machali, ametoa mwezi mmoja kwa Halmashauri ya Wilaya hiyo kupeleka ofisini kwake orodha ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambavyo vilikopeshwa shilingi milioni 230 na baadhi kushindwa kuzirejesha.

Alitoa agizo hilo kutokana na kuwepo kwa hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), katika hesabu zilizoishia Juni 30 mwaka jana, ambayo ilijadiliwa katika mkutano maalumu wa Baraza la Madiwani.

Kwenye mkutano huo wa Baraza la Madiwani Mkuu huyo wa Wilaya alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali Charles Mbuge.

"Ifikapo Julai 22 mwaka huu niwe nimepata taarifa mezani kwangu pamoja na orodha ya vikundi ambavyo havikulipa ili hatua zichukuliwe na fedha za serikali zirejeshwe ili ziwanufaishe wengine, haiwezekani watu wanapewa mikopo wanakula hela na kukaa kimya lazima zirejeshwe," alisema Machali.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, Fatna Laay alivitaka vikundi vinavyopewa mikopo hiyo kuheshimu makubaliano na kurejesha kwa wakati na kuwa siyo busara kukopeshwa na kwenda kudaiana mahakamani.

"Ukipata shida sema kwamba jamani rejesho hili nimekwama kwa sababu fulani lakini ujitahidi kurejesha usilimbikize, lakini pia msinunue vitenge na nguo za watoto kwa fedha hizi na badala yake zitumieni kuzalisha zingine ziongeze kipato katika familia na hilo ndilo lengo la serikali," alisema Laay.

Hata hivyo, pamoja na agizo la Mkuu wa Wilaya ya Bukoba la kufuatiliwa kwa vikundi ambavyo vimeshindwa kurejesha mikopo, siku hiyo pia vikundi vingine 32 vilipatiwa mikopo yenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 119.

"Vikundi 22 vya wanawake, saba vya vijana na vitatu vya watu wenye ulemavu vimekidhi kupata mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 119, katika kipindi hiki cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2021/2022,

Halmashauri imechangia shilingi milioni 30 kutoka katika vyanzo vyake vya ndani vya mapato na shilingi milioni 89.5 kutoka kwenye akaunti ya marejesho ya mikopo," alisema Ofisa Maendeleo ya Jamii, Felista Shayo.

Akizungumza baada ya kupokea mfano wa hundi ya mikopo hiyo, mmoja wa wanufaika Erick Christopha, aliwaasa wanavikundi wenzake kutumia fedha wanazokopeshwa kulingana na malengo yao ili kuepuka kuzitumia vibaya na baada kukwama na kushindwa kurejesha.

"Vikundi vingine wanashindwa kurejesha kwa sababu wanachukua fedha kwa lengo la kwenda kugawana kila mmoja afanye kazi yake binafsi, wengine badala ya kufanyia biashara wanatumia pesa katika mambo ya starehe, kwa hiyo kwa namna hiyo unaweza kujikuta unakwama," alisema Christopha.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AMINA SALUM SALUM** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **SUZUKI ESCUDO** yenye usajili namba **T531 DDH** yenye CHASSIS NAMBA: **TD54W106939,** ENGINE NAMBA: **J20A2563741**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/URRQ/RB/234778/2022**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**MARY ALLY SELEMAN** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE289710** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam 2020. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu naye.

**POLISI TAARIFA: DSM/PHQ/RB/207733/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABRAHAM JAMES GONDWE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA CRESTA YENYE NAMBA ZA USAJILI T.229 AZS.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.**TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/248429/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AHMED MAHMOUD SAID** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA NISSAN PATROL YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 201 BGS.** YENYE CHASSIS **NO. JNITDSY61U0300979** NA ENGINE **NO.PD42049926** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

**TAARIFA YA POLISI KAH /RB/ 328/2022**

**JUMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA**
**KATIKA BARAZA LA KATA-TINDE LILILOPO TINDE SHINYANGA.**
**SHAURI NAMBA; 07/2022**
**MORY ONESMO KABENDERA................MLALAMIKAJI**
**DHIDI YA**
**ROBERT NKWABI MAGEME.................MLALAMIKIWA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

Mlalamikiwa uliyetajwa hapo juu (Robert Nkwabi Mgeme); unaamriwa kufika Barazani kujibu shauri husika linalokukabili siku ya Jumatatu tarehe 27/6/2022 saa 3.00 Asubuhi.
Unaamriwa kuhudhuria bila kukosa pamoja na ushahidi au vielelezo vyovyote vinavyotokana na shauri hilo ili kurahisisha upatikanaji wa haki.
Kumbuka kwamba, usipohudhuria shauri hilo litasikilizwa na kutolewa uamuzi bila ya wewe kuwepo.

**Imetolewa tarehe 22/6/2022 na mimi**

KATIBU WA BARAZA LA KATA TINDE.

**BONIFACE MHANA**
**KATIBU**
**BARAZA LA KATA-TINDE**
**SHINYANGA**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MATHA AMINIEL MARIKI** anatangaza kupotelewa na cheti cha Master of arts (ma) health policy and management chenye no. **HD/MUH/T.57/2008.** Kilichotelewa na **MUHIMBILI UNIVERSITY OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES** mwaka 2010. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/248333/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DIOCESE OF WESTERN TANGANYIKA - KASULU** inatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili T 139 CAK – NISSAN TERRANO. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Taarifa ya Polisi: KAS/RB/1750/2022.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**RIFAT HASHMAT BAIG a**natangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1187-0106** kilichotolewa na Baraza La mitihani la Taifa kupitia **ST.MARY GORETI SECONDARY SCHOOL** mwaka **2016** na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S.1187-0688 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST. MARY GORETI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/CHU/RB/237593/2022**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

Ndugu **WILSON ELIAS BAHANZIKA** anatangaza kupotelewa na kadi mbili za pikipiki, Honda Cd yenye namba za usajili **T683 AHA** na Bajaj Boxer yenye namba za usajili **MC 179 AXT**. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/245683/2022.** Kwa yeyote atakayezionа atoe taarifa polisi au apige simu namba **0713991407.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 810 YA 2022**
**RESTUTA ABASI SAULO..........................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**EDGAR ZAKARIA.........................................MJIBU MAOMBI**
**CHARLES MWENDIPANDO........................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

**EDGAR ZAKARIA** Popote ulipo Unaarifiwa Ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe **06/07/2022** mbele ya Mwenyekiti E.Mogasa wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

**Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 21.06.2022.**

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**

MOROGOROkadi ya gari aina ya Toyota Harrier yenye no za usajili T837DJX, ENGINE NO 2AZB178269 Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi,

**Taarifa ya Polisi: DOD/DOD/RB/249594/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ROSEMARY JOHN MISOLO**, Anatangaza kupotelewa na cheti cha Kidato cha Nne chenye **Index no S.4847/0026** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia shule ya Peace Land Sekondary School Mwaka 2015. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi
**POLISI TAARIFA: DOD/DOD/RB/192836/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IZACK CHOGERO MWIMBA,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Harrier yenye no za usajili **T837DJX**, ENGINE NO **2AZB178269** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi,

**Taarifa ya Polisi: DOD/DOD/RB/249594/202**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-11

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Basi mwenzangu." Siwatu alianza kumhadithia wifi yake, mpenzi wa kaka yake Dibwela.

"Usiku nimelala, nikasikia kama mtu anavunja mlango, kabla sijafanya kitu chochote naona mtu anaingia amejificha uso, nikajua nimekufa hapa, si ndiyo akanikaba shingoni akanitupia kitandani akanibaka." Akamalizia na sauti ya huzuni akaanza kulia.

"Basi Siwatu, basi wifi yangu, ni mitihani tu ya maisha, yatapita tu haya..."

"Kinachoniuma mimi Mpaje kwa nini anibake? Nimemkosea nini? Kwani mimi nimefanya baya gani hapa kijijini?"

"Hivi hadi anaondoka hukumjua ni nani?"

"Kwani alivyoondoka mimi nilikuwa mzima? Nilishazimia, angetaka hata kuniua angeniua. Na nilijaribu sana kutaka kumvua ile kofia yake kama ninja usoni na ile miguo yake, ili nihisi tu anaweza kuwa nani, lakini nilishindwa, alitumia nguvu nyingi kuhakikisha simfahamu. Kusema kweli wifi atakuwa ni mwanaume ambaye ananifahamu na mimi namfahamu..."

"Basi nyamaza wifi, kaka yako anakuja." Mpaje alimnong'oneza Siwatu.

Ni wakati huo huo, Dibwela alikuwa ameingia. Alionekana kukasirika kidogo.

"Vipi mwenzetu, mbona hivyo?" Mpaje akamuuliza mpenzi wake.

"Wananikera sana, sijui wanaona kwa sababu huyu ni yatima? Wiki imepita sasa, nimesharipoti kwa Mwenyekiti wa Kijiji aliyefanya tukio hili asakwe haraka, apatikane apelekwe kwenye vyombo vya sheria, lakini naona sielewi, mpaka leo hakuna kinachofanyika."


"We kaka si uache tu, kama wao hawataki, wala usihangaike, mimi sasa hivi hali yangu inaendelea vizuri..."

"Hakuna kitu kama hicho Siwatu, nitahakikisha kuwa yeyote aliyefanya hivi nakula naye sahani moja, kwa hili wewe kaa pembeni, niachie mimi."

"Dibwela, inawezekana aliyefanya hivyo ni mtu kutoka mbali, Mwenyekiti atafanyaje?"

Dibwela akacheka kicheko ambacho si halisi. Siyo cha furaha, bali ni cha uchungu na hasira.

"Mimi nina akili kuliko unavyofikiria, mtu kutoka mbali, au vijiji jirani asingevaa maguo ya kujificha kama ninja, huyo aliyefanya hivyo ni kwamba anamfahamu dada yangu na pia Siwatu anamfahamu, ndiyo maana ameamua kufanya hivyo kwa hofu ya kujulikana. Aliyefanya kitendo hicho yumo humu humu kijijini. Atafutwe na kukamatwa haraka sana. Kesho namfuata tena mwenyekiti." Dibwela alisema.




**"Kinachoniuma mimi Mpaje kwa nini anibake? Nimemkosea nini? Kwani mimi nimefanya baya gani hapa kijijini?"**

*********************************

Wanakijiji walikuwa wamekusanyika. Ni kikao cha ghafla kilichoitishwa jana yake jioni. Hakuna yeyote aliyejua kilihusu nini.

Mwenyekiti alivaa mawani yake, mkononi akiwa na makaratasi kadhaa ambayo alikuwa ameyashika.

"Wanakijiji wa Semwanza, mmeitwa hapa kutokana na mambo yanayohusu kijiji chetu. Mara nyingi huwa tunaitana kwa sababu za kimaendeleo, misiba, sherehe, tatizo, au chochote kile ambacho kimesibu kijijini au mwanakijiji.

Hivi karibuni mwanakijiji mwenzetu mmoja ambaye hapa hayupo, kwa sababu za kimaadili tumemwambia apumzike tu. Anaitwa Siwatu, aliingiliwa na mtu asiyejulikana aliyevunja mlango wa nyumba yake na kumfanyia kitendo kibaya ambacho kilisababisha alazwe kwenye zahanati hapo jirani.

Kutokana na tukio hilo, uongozi wa kijiji uliona si vema kuendelea kukaa bila kufanya uchunguzi na kujua ni kipi hasa kimetokea na ni nani aliyefanya hivyo. Huo sasa utakuwa si uongozi kwa sababu kama ikiachiwa kesho atafanyiwa mtu mwingine na mwingine, uongo kweli?" "Kweliii..." Wakaitikia wanakijiji kwa pamoja.

"Kwa hivyo basi, tukafanya uchunguzi na vyanzo vyetu, hatimaye tumempata mtu ambaye aliyesababisha jambo hilo."

Alipofika hapo, hakuna tena aliyemsikiliza bali kulikuwa na minong'ono ya wanakijiji wao kwa wao, haikujulikana ni kitu gani walikuwa wakiongea au kunong'onezana. Halafu wakanyamaza ili kumjua mtu huyo.

"Nimtaje?" Mwenyekiti akauliza "Mtajeee..."

"Kwa bahati nzuri au mbaya mtu aliyefanya kitendo hiki alishawahi kuja hapa na tukaishi naye hapa hapa, tukamfanyia wema mkubwa, lakini malipo yake leo yamekuwa haya."

Wanakijiji wakawa kimya, ukimya ambao hata ukitupa sindano unaweza kuisikia.

"Mtu huyu ni Bakari." Akamtaja na alipomaliza akakunja karatasi zake akabaki amesimama akiwaangalia wanakijiji wake ambao walionekana kupigwa na butwaa.

Kulikuwa na mikono kadhaa iliyonyooshwa wakitaka kuuliza maswali, lakini waliokaa pembeni kwa mwenyekiti walidai muda umekwenda.

"Huyu mtu anaishi Msata, kwa hiyo wala si ajabu kutoka huko na kuja kufanya unyama huu na kukimbia. Inawezekana alikuwa na nia yake tangu zamani, inawezekana amefanya hivyo kutokana na kushauriwa na waganga wa kienyeji." Mwenyekiti bado alikuwa akiitetea hoja yake ili iwe na mashiko.

"Na baada ya hapo naufunga mkutano hadi hapo tutakapokutana tena."

Wanakijiji ni kama vile waliachwa njia panda. Wengine waliamini na wengine hawakuamini.

"Yaani kweli yule ni mpenzi wake, wamekaa hapa chini ya paa moja miezi mitatu, halafu kweli aje kumbaka kweli akiwa amejifunika manguo kweli?" Akahoji mama mmoja wakati wakirejea na wenzake mkutanoni.

"Mwenyekiti leo katufunga kamba, mtu atambakaje mpenzi wake?. Halafu kaondoka miezi kibao sasa aje usiku kumbaka? Hivi wale wanavyopendana, hasa Siwatu alivyokuwa anampenda Bakari angekuja tu hivi hivyo angechinjiwa mpaka kuku, leo aje vile, afanye vile, ili iwe nini?" Kijana mmoja akawaambia wenzie, mmoja akajibu.

"Mimi nawaambia wale wameona aibu. wiki ngapi sasa hawajampata aliyefanya kitendo hicho. Kijiji kinapiga kelele, wakaona wakae wamtafute mtu ambaye hayupo wambambikie kesi ili wao wawe salama, waondokane na lawama." Wengi wakakubaliana na hilo.

"Jamani, lakini mimi taarifa za ndani nilipata kusikia, wale hawakuwa wapenzi, walikuwa wanaishi nyumba moja, lakini mmoja analala chini, Siwatu kitandani hadi alipoondoka, na hilo ameshawahi kuniambia mwenyewe Siwatu, inawezekana akapatwa na tamaa, akaja kwa njia ile." Msichana mmoja alitoa siri ambayo haikukubaliwa kwa asilimia tisini. Wengine wakacheka.

"Yaani wale hawakuwa mtu na mpenzi wake kweli? Kawadanganye watoto wadogo. Jinsi walivyokuwa wakiongozana mtaani tu kama kumbikumbi walionyesha kabisa kama ni mtu na mpenzi wake. Mimi nasema hivi, mbakaji hapa hajapatikana, mwenyekiti na kamati yake wametudanganya."

Ilikuwa ni mitazamo ya wanakijiji baada ya mwenyekiti kudai ni Bakari aliyeonekana kuwa ni mpenzi wa Siwatu, kwa kukaa kijijini hapo kwa miezi mitatu, baada ya kuokotwa porini akiwa na majeraha, akinusurika kifo.

Na yeye aliyemuokoa, ndiye aliyembaka.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# IHEFU YAMNASA WADADA IKIJIIMARISHA NA LIGI KUU

**Na Saada Akida**

KATIKA kuimarisha kikosi chake kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, klabu ya Ihefu imekamilisha usajili wa aliyekuwa beki wa Azam FC, Nicholas Wadada, imefahamika.

Ihefu ndio mabingwa wa Ligi ya Championship msimu wa 2021/2022 huku nafasi ya pili ikishikwa na DTB FC (sasa Singida Big Stars), ambazo zimepanda daraja moja kwa moja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Ihefu FC, Zagalo Chalamila alisema Wadada amesaini mkataba wa mwaka mmoja na wanaamini ujio wake utasaidia kuimarisha safu ya ulinzi ya timu hiyo.

Chalamila alisema usajili wa beki huyo ni mapendekezo ya benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Zuberi Katwila ambaye pia ameweka wazi anahitaji kuongezewa mshambuliaji na beki mwingine.

"Wadada ni mali ya Ihefu rasmi na sasa tunaendelea na mchakato wa usajili wa beki na mshambuliaji, tunaaangalia zaidi hapa nyumbani, tunaangalia zaidi wachezaji wazoefu ili waje kusaidia timu yetu katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Chalamila.

Aliongeza mbali na nafasi hizo pia wako katika mchakato wa kuangalia wachezaji wengine kwa kusubiri msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara ufikie tamati ili nyota wengi wawe huru kufanya mazungumzo kwa ajili ya kupata huduma zao.

"Kuhusu benchi la ufundi bado tunaendelea na Katwila baada ya bodi ya wakurugezi kukaa na kufikia uamuzi huo na kumpa majukumu ya usajili ya kuimarisha kikosi chetu kuelekea msimu ujao," alisema Chalamila.

Alisema pia kulingana na yaliyotokea msimu uliopita hawataki kuona yanarejea kwa kuhakikisha wanafanya usajili wa wachezaji watakaosaidia timu hiyo kuleta ushindani.

Kiongozi huyo alisema wanatarajia timu yao kuweka kambi maalumu ya kujiandaa na msimu mpya na kucheza mechi mbalimbali za kirafiki dhidi ya klabu za ndani na nje ya Tanzania.




Mshambuliaji wa timu ya vijana ya umri chini ya miaka 17 ya KMC (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya nyota mwenzake wa Pan African katika mechi ya Ligi ya U-17 iliyochezwa juzi jijini Dar es Salaam. KMC ilishinda mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

# Biashara yapania kuimaliza KMC

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikiwa imefungiwa kusajili nyota wapya kwa misimu miwili, kikosi cha Biashara United kimepania kuondoka na ushindi ili kurejesha matumaini ya kubakia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara leo kwa kuikaribisha KMC kwenye Uwanja wa Karume mkoani Mara.

Kocha Mkuu wa Biashara United, Khalid Adam alisema jana wachezaji wake wamefanya mazoezi vyema kuelekea kwenye mechi hiyo, lakini pia amejaribu kuwaeleza juu ya umuhimu wa mechi hiyo.

"Tumefanya mazoezi muhimu kutokana na aina ya mechi yenyewe tunayokwenda kucheza, pia tunajaribu kukaa mara kwa mara na vijana kuwaeleza umuhimu wa mchezo huo, wanatakiwa kupambania ili wahakikishe wanashinda kwa ajili ya kuinusuru timu," alisema kocha huyo.

Ramadhani Chombo 'Redondo', mchezaji wa timu hiyo alisema kila mchezaji anajua umuhimu wa mechi hiyo na wana imani watashinda kwa sababu wanacheza nyumbani.

Naye nahodha wao, Abdulmajid Mangalo alikiri timu yao ipo kwenye hali mbaya lakini mechi mbili zilizobaki watahakikisha wanafanya kila njia ili kupata pointi sita zitakazowaondoa kwenye eneo la hatari.

Biashara United inashika nafasi ya 15 katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 25 mkononi.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya Coastal Union dhidi ya Kagera Sugar wakati Polisi Tanzania wataivaa Geita Gold, Mbeya Kwanza wataikaribisha Ruvu Shooting, Azam watakuwa ugenini dhidi ya Dodoma Jiji na mabingwa Yanga watawakabili Mbeya City.

## Wazazi watakiwa kuendeleza vipaji

**Na Maulid Mmbaga**

MMOJA wa Wakurugenzi wa Shule za St.Mary's, Mutta Rwakatare, ametoa wito kwa wazazi na walezi kuwaendeleza na kuwawekea mazingira mazuri watoto wao baada ya kubaini wanavipaji ili wafikie malengo yao.

Rwakatare alitoa wito huo katika hafla ya bonanza lililofanyika kwenye Uwanja wa Kenton ambapo wanafunzi wa shule ya msingi na sekondari ya East Africa walipata fursa ya kuonyesha vipaji vyao kwa kushiriki michezo mbalimbali kama mpira wa miguu, kuimba na kuruka kamba.

Alisema kila mwanafunzi ana malengo, ikiwamo kuwa mwalimu, daktari, rubani, wanariadha, wachezaji kandanda kama Samata (Mbwana) au wanamuziki kama Hormonize, hivyo alisisitiza wazazi endapo ataona mtoto anapendelea kitu fulani nje ya masomo asimnyime badala yake amuendeleze.

"Niwashukuru walimu mnafanya kazi kubwa, tunaahidi kuweka miundombinu mizuri ya michezo, wazazi msiwe na hofu kutushauri na kutuambia pale ambapo tutakuwa tumekosea ili tujirekebisha, hii ni shule yenu sio yetu na wala sio ya mwalimu, tushirikiane kwa ajili watoto wetu wafikie malengo," alisema Rwakatare.

Salum Saidi, mmoja wa wazazi wa walioshiriki bonanza hilo alisema katika baadhi ya maeneo mazingira ya kuwezesha michezo bado ni finyu, hivyo alitoa wito kwa wadau wa elimu na michezo kuboresha miundombinu itakayowawezesha wanafunzi kushiriki michezo mbalimbali.

## Bandari yatwaa ubingwa netiboli

**Na Cheji Bakari,TANGA**

TIMU ya Bandari imefanikiwa kuibuka mabingwa wa Ligi ya Netiboli ya Wilaya ya Tanga Mjini baada ya kuwafunga majirani zao, Halmashauri ya jiji hilo.

Ligi hiyo iliyokuwa inachezwa katika viwanja vya Magereza jijini hapa ilimalizika rasmi juzi.

Bandari ilifanikiwa kutwaa ubingwa huo baada ya kuicha Halmashauri ya Jiji magoli 39-34.

Timu zilizoshiriki katika ligi hiyo zilikuwa ni saba ambapo nyingine ni pamoja na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga Uwasa), Kiomoni, Bandari Kings (Wanaume), Swahili na Chuo cha Utumishi Kampasi ya Tanga.

Aidha kwa upande wa timu za netiboli wavulana, Bandari Kings ilibuka kidedea baada ya kupata ushindi wa magoli 22-13 dhidi ya Chuo cha Utumishi wa Umma.

## ZISIKUPITE

### LEWANDOWSKI SOKONI
KLABU ya Barcelona hatimaye wamewasilisha ombi la kumnunua mshambuliaji wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33, ambalo lina thamani ya hadi pauni milioni 34. ***(Telegraph)***

### RAPHINHA ANUKIA ARSENAL
ARSENAL wanakaribia kumsajili mshambuliaji wa Brazil, Raphinha kutoka Leeds United, huku nia ya Barcelona kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ikiwa imepungua. ***(Goal)***

### RICHARLISON AGOMBEWA
CHELSEA wameungana na Tottenham Hotspur kutaka kumsajili mshambuliaji wa Brazil, Richarlison kutoka Everton, ambao wanataka zaidi ya pauni milioni 50 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Mail)***

### CHELSEA KUPATA PIGO
MARINA Granovskaia, ambaye alichukua jukumu la uhamisho wa wachezaji katika wa Chelsea chini ya mmiliki wa zamani, Roman Abramovich, anakaribia kuondoka katika klabu hiyo. ***(Guardian)***

### BROJA MAMBO MAZURI
KLABU ya West Ham inatazamiwa kutoa takriban pauni milioni 30 kwa mshambuliaji wa Chelsea na Albania, Armando Broja mwenye umri wa miaka 20, ambaye alicheza kwa mkopo Southampton msimu uliopita. ***(Sky Sports)***

### SPURS YAMFUATA ERIKSEN
KLABU ya Tottenham Hotspur iliwasiliana na kambi ya mchezaji wa Denmark, Christian Eriksen wiki chache zilizopita, lakini hawajaonyesha tena nia ya kumtaka mchezaji wao huyo wa zamani mwenye umri wa miaka 30, ambaye alitumia kipindi cha pili cha msimu uliopita huko Brentford. ***(Football London)***

### DE JONG ANUKIA UNITED
KOCHA mpya wa Manchester United, Erik ten Hag ameiambia klabu hiyo anataka kuwasajili Christian Eriksen na kiungo wa kati wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Frenkie de Jong (25). ***(Goal)***

### UNITED YAMFUATA EVANILSON
KLABU ya Manchester United imekuwa na ofa ya pauni milioni 55 kwa mshambuliaji wa Brazil, Evanilson iliyokataliwa na Porto, lakini klabu hiyo ya Old Trafford inapanga kutoa ofa mpya kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(O Jogo, via Mail)***

### ARSENAL, UNITED VITANI
BAADA ya kushindwa kumsajili mlinzi, Jurrien Timber mwenye umri wa miaka 21, Manchester United inaweza kuchukua hatua ya kumsajili mchezaji mwenzake wa Ajax, Lisandro Martinez (24). Beki huyo wa kati wa Argentina pia analengwa na Arsenal. ***(Mirror)***

### VILLA KUMUUZA MCGINN
KLABU ya Aston Villa ipo tayari kusikiliza ofa kwa kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Scotland, John McGinn mwenye umri wa miaka 27, msimu huu wa joto. ***(Football Insider)***

### TREZEGUET NJIA MOJA
WINGA wa Timu ya Taifa ya Misri, Trezeguet mwenye umri wa miaka 27, anakaribia kuondoka Aston Villa na kujiunga na Trabzonspor ya Uturuki kwa takriban pauni milioni tatu. ***(Mail)***

### COOPER MAMBO MAZURI
KOCHA wa Nottingham Forest, Steve Cooper, ambaye alikiongoza kikosi chake kupanda Ligi Kuu England msimu uliopita, yuko mbioni kusaini mkataba mpya wa muda mrefu na klabu hiyo. ***(Nottinghamshire Live)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR ALITAKA TAJI LA ULAYA AKIWA PSG

Afunguka hiyo ndio ndoto yake licha ya kuwapo na uvumi wa...

**PARIS, Ufaransa**

WAKALA wa zamani wa Neymar, Wagner Ribiero anaamini Mbrazil huyo hayuko tayari kuondoka Paris Saint-Germain kwa sababu bado ana ndoto ya kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na vigogo hao wa Ufaransa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 ana mkataba hadi mwaka 2025, lakini kumekuwa na uvumi PSG wanaweza kutaka kumtoa baada ya kumsajili Lionel Messi mwaka 2021 na hivi karibuni kurefusha mkataba wa Kylian Mbappe.

Kurejea Barcelona kumezimwa kwa muda mrefu kwa Neymar, ambaye alishinda naye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2014-15, huku pia aliwahi kuzungumzia nia yake ya kucheza Marekani.

Hata hivyo, alipoulizwa kuhusu mustakabali wa Neymar, Ribiero aliweka wazi anaelewa nyota huyo wa zamani wa Santos hafikirii kuondoka na ameelekeza macho yake kuhitimisha kusubiri PSG kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Neymar ana ndoto kuwa bingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na PSG," aliiambia Goal.

"Licha ya uvumi wote kuhusu uwezekano wa kuondoka, ana motisha sana na hataacha hadi afanikishe."

Alipoulizwa kama Neymar anapenda mradi huo PSG, aliongeza: "Bila shaka. Kila mwaka unaopita Nasser Al-Khelaifi (rais wa klabu) anaboresha timu kwa kila namna.

"Wamemaliza tu kituo cha mazoezi, ambacho kitakuwa mojawapo ya bora zaidi. Na sasa anataka kuwa na wachezaji bora wa Ufaransa katika PSG."

Tangu Neymar ajiunge na PSG mwaka wa 2017, wababe hao wa Ufaransa wametolewa katika hatua ya robo fainali katika misimu mitatu kati ya mitano - wakimaliza washindi wa pili 2019-20 na kutinga nusu fainali mwaka uliofuata.

Katika kipindi hicho, Neymar amefunga mabao 20 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kupata asisti 13 - huku mchezaji pekee aliyetoa pasi nyingi zaidi katika kipindi hicho akiwa Mbappe.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,008,5

MECHI KALI
MBEYA CITY
VERSUS
YOUNG AFRICANS
1 | 4.61
X | 3.04
2 | 1.80

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RONALDO ANATAKA KUONDOKA UNITED



**MANCHESTER, England**

RIPOTI zinasema nyota wa kimataifa wa Ureno, Cristiano Ronaldo anataka kuondoka Manchester United.

Kwa mujibu wa ripoti ya gazeti la kila siku la michezo la Hispania la AS, Bayern Munich inaangalia uwezekano wa kumsajili mshambuliaji huyo wa kireno iwapo Robert Lewandowski ataondoka Bavaria.

Ripoti hiyo imedai ni wazi wakati wa Ronaldo kwa Manchester United 'umefikia mwisho'.

Madai hayo yamekuja ingawa kwa sasa Bayern Munich haina nia ya kumuuza Lewandowski licha ya kumsajili, Sadio Mane.

Barcelona imeripotiwa kutuma ombi la ada ya Euro milioni 40 sawa na zaidi ya shilingi bilioni 98, hapo June 23, mwaka huu kwa ajili ya kumsajili Lewandowski.

# Zidane afunguka amepokea ofa

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane ameshindwa kukanusha juu ya kuhusishwa kwake na klabu ya Paris Saint-Germain na kusisitiza anaweza kwenda kwenye klabu mbili au tatu.

Kwa mujibu wa Fabrizio Romano, Zidane alinukuliwa na L'Equipe akisema, kama kocha wa kiwango chake, kuna kazi chache tu zinazomfaa na hizo itakuwa ni ujinga kukataa moja kati ya klabu kubwa barani Ulaya.

"Kamwe usiseme hapana, kama meneja, hakuna klabu 50 ambazo ninaweza kwenda. Kuna uwezekano wa klabu mbili au tatu," alisema Zidane

Zidane alikuwa akitajwa kwenye orodha ya warithi wa kuchukua nafasi ya Mauricio Pochettino pale Parc des Princes msimu huu wa joto.

Lakini inaonekana kuna jambo tofauti wakati PSG wakiwa wamemgeukia kocha wa Nice, Christophe Galtier.

Rekodi ya ushindi ya Galtier ni ya kuvutia - aliiongoza Lille kutwaa taji la Ligue 1 msimu wa 2020/21, akishinda PSG katika wakati huo.

Lakini rekodi ya Zidane ni mara dufu, haswa kwa Ulaya na Mfaransa huyo aliiongoza Real Madrid kutwaa mataji matatu mfululizo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kati ya 2016 na 2018, jambo ambalo hakuna kocha aliyefanikiwa katika zama hizi.



HABARI MICHEZO

534,842/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/06/22 | 22:10 | Club Atletico Alvarado vs Belgrano | 3.50 | 2.90 | 2.33 |
| 02. 25/06/22 | 22:30 | Atletico PR vs Bragantino SP | 2.44 | 3.03 | 3.08 |
| 03. 26/06/22 | 00:00 | DC United vs Nashville | 2.43 | 3.40 | 2.85 |
| 04. 26/06/22 | 00:00 | Colon Santa Fe vs Huracan | 2.35 | 3.28 | 3.13 |
| 05. 26/06/22 | 02:30 | Toronto vs Atlanta United | 2.96 | 3.51 | 2.32 |
| 06. 26/06/22 | 05:00 | San Jose Earthquake vs Los Angeles Galaxy | 2.61 | 3.56 | 2.56 |
| 07. 26/06/22 | 05:30 | Portland Timbers vs Colorado Rapids | 2.26 | 3.43 | 3.12 |
| 08. 26/06/22 | 12:00 | Vissel Kobe vs Urawa Red Diamonds | 2.78 | 3.23 | 2.63 |
| 09. 26/06/22 | 12:00 | Nagoya Grampus vs Kashima Antlers | 2.92 | 3.28 | 2.48 |
| 10. 26/06/22 | 12:00 | Yokohama vs Niigata Albirex | 2.59 | 3.24 | 2.74 |
| 11. 26/06/22 | 12:30 | Kyoto Sanga vs Shonan Bellmare | 2.73 | 3.29 | 2.63 |
| 12. 26/06/22 | 13:00 | Omiya Ardija vs Zwiegen Kanazawa | 2.91 | 3.21 | 2.48 |
| 13. 26/06/22 | 19:00 | Ham-Kam vs Sarpsborg | 2.74 | 3.43 | 2.45 |
| 14. 26/06/22 | 19:00 | Sandefjord vs Tromso | 2.78 | 3.42 | 2.42 |
| 15. 26/06/22 | 19:00 | Stromsgodset vs Lillestrom | 2.73 | 3.42 | 2.46 |
| 16. 26/06/22 | 19:00 | San Lorenzo vs Tigre | 2.84 | 3.30 | 2.54 |
| 17. 26/06/22 | 22:00 | Botafogo RJ vs Fluminense | 2.52 | 3.12 | 2.87 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 25/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1268 | Kawasaki Frontale vs Jubilo Iwata | 1.42 | 4.33 | 6.10 |
| 13:00 | 3418 | Sandviken vs Nordstrand | 4.04 | 4.43 | 1.60 |
| 13:00 | 3788 | Roasso Kumamoto vs Oita Trinita | 2.44 | 3.05 | 2.76 |
| 13:00 | 4724 | Suwon City vs Suwon Samsung | 2.50 | 3.09 | 2.65 |
| 14:00 | 1041 | Anyang vs Seoul E Land | 1.98 | 3.29 | 3.44 |
| 14:00 | 4553 | FC Seoul vs Incheon Utd | 1.89 | 3.24 | 3.83 |
| 14:00 | 4629 | Okzhetpes vs Igilik | 1.14 | 6.85 | 13.70 |
| 14:30 | 5346 | Tianjin Teda vs Meizhou Kejia | 3.00 | 3.10 | 2.25 |
| 14:30 | 5510 | Hangzhou NG vs Shandong Luneng | 5.29 | 3.77 | 1.55 |
| 14:30 | 5701 | Wuhan Zall vs Shanghai SIPG | 4.81 | 3.68 | 1.61 |
| 15:00 | 1290 | Taraz Karatau vs Fk Shakhtar Bulat | 1.22 | 5.69 | 9.81 |
| 15:00 | 1466 | Steinkjer vs Kolstad | 7.46 | 5.69 | 1.27 |
| 15:00 | 1561 | Kairat-Zhastar vs Kaisar Kyzylorda | 4.70 | 4.02 | 1.57 |
| 15:00 | 1594 | Brodd vs Djerv 1919 | 2.05 | 4.12 | 2.70 |
| 15:00 | 1952 | Rana FK vs Strindheim IL | 3.14 | 4.12 | 1.86 |
| 15:00 | 2104 | Floro vs Lillehammer FK | 1.60 | 4.20 | 4.20 |
| 15:00 | 3527 | Isloch vs Gomel | 2.31 | 3.35 | 2.71 |
| 15:00 | 3754 | Pors Grenland vs Express IL | 1.06 | 9.81 | 18.63 |
| 15:00 | 4116 | FK Ekibastuz vs Yassi Turkistan | 2.12 | 3.35 | 3.20 |
| 15:30 | 2807 | Gvvv vs Kozakken Boys | 2.11 | 3.38 | 3.04 |
| 16:00 | 1939 | Polisi Tanzania vs Geita Gold FC | 2.24 | 2.70 | 3.53 |
| 16:00 | 2458 | Mbeya Kwanza FC vs Ruvu Shooting | 2.20 | 2.79 | 3.48 |
| 16:00 | 2523 | Biashara United vs KMC | 1.71 | 3.01 | 5.52 |
| 16:00 | 3445 | Akzhaiyk Uralsk vs Ordabasy | 2.66 | 2.86 | 2.66 |
| 16:00 | 3905 | Mbeya City vs Young Africans | 4.61 | 3.04 | 1.80 |
| 16:00 | 3919 | Magni vs Reynir Sandgerdi | 1.64 | 4.61 | 3.68 |
| 17:00 | 1076 | Haugesund vs Viking | 3.46 | 3.71 | 1.94 |
| 17:00 | 3759 | IF Vestri vs UMF Grindavik | 2.21 | 3.69 | 2.65 |
| 17:00 | 5162 | Mjolner vs Skjervoy | 1.49 | 4.61 | 4.71 |
| 17:00 | 5595 | Slutsk vs Vitebsk | 2.23 | 3.00 | 3.14 |
| 17:00 | 5713 | Orkla vs Melhus | 1.48 | 4.91 | 4.51 |
| 18:00 | 5200 | Al Sareeh vs AL Salt | 2.65 | 2.84 | 2.70 |
| 18:00 | 5478 | Aksu vs Shakhter Karagandy | 2.51 | 3.15 | 2.61 |
| 19:00 | 2264 | NSI Runavik vs Vikingur Gota | 5.50 | 4.52 | 1.43 |
| 19:00 | 2939 | Rosenborg vs Kristiansund | 1.41 | 4.82 | 6.42 |
| 19:00 | 4574 | Dodoma FC vs Azam | 2.83 | 2.73 | 2.63 |
| 20:00 | 2750 | Sochi vs Zenit St Petersburg | 5.49 | 4.12 | 1.48 |
| 20:00 | 4388 | Hartford Athletic vs Louisville City | 3.72 | 3.82 | 1.75 |
| 20:10 | 5142 | Deportivo Moron vs Gimnasia Jujuy | 2.09 | 2.84 | 3.72 |
| 20:30 | 2808 | Faisaly Amman vs Wihdat Amman | 3.24 | 2.75 | 2.34 |
| 21:00 | 5445 | Neman Grodno vs BATE Borisov | 3.58 | 3.19 | 1.97 |
| 21:30 | 1787 | Central Ballester vs Yupanqui | 2.36 | 2.79 | 3.14 |
| 21:30 | 2444 | Canuelas vs Talleres RDE | 2.46 | 2.81 | 2.96 |
| 21:30 | 3478 | CA Lugano vs Club Mercedes | 2.37 | 2.74 | 3.19 |
| 21:30 | 5218 | Talleres vs Central Cordoba | 2.28 | 3.00 | 3.05 |
| 22:00 | 3833 | CSD Barnechea vs Cobresal | 2.89 | 3.28 | 2.22 |
| 22:00 | 4639 | Seattle Sounders vs Sporting Kansas City | 1.74 | 3.82 | 4.48 |
| 22:30 | 3089 | Atletico Pr vs Bragantino SP | 2.43 | 2.96 | 2.86 |
| 22:30 | 5135 | Spain W vs Australia W | 1.54 | 3.79 | 5.31 |
| 23:30 | 1978 | Sporting Cristal vs Alianza Atletico | 1.42 | 4.51 | 5.69 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KOCHA MTIBWA AMKUBALI SAKHO, TIMU YAKE IKIPOTEA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Mtibwa Sugar, Awadh Juma amewataka wachezaji wazawa kujifunza kwa kiungo wa Simba, Pape Sakho kutokana na uwezo mkubwa wa soka na kufikiri anaoufanya kwa sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wakati kocha huyo akisema hayo, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Selemani Matola amesema viwango vya Sakho na Peter Banda vimeongezeka kutokana na kuwaachia kucheza huru.

Wakizungumza baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara juzi, kati ya timu hizo mbili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na Simba kuibuka na ushindi mabao 2-0, makocha hao kila mmoja alimzungumzia Sakho ambaye kwa siku ya karibuni amekuwa kwenye kiwango cha juu tangu asajiliwe msimu huu akitokea Teungueth FC ya nchini Senegal.

"Ni mara ya tatu nadhani sasa anafunga goli la aina hii, hata mechi iliyopita dhidi ya KMC alifunga goli linalofanana na hili, huu ni ukomavu wa akili ya mchezaji wa kujua ni muda gani na nifanye nini. Sisi mwanzoni tumepata nafasi nyingi lakini tumezipoteza, ya Sakho haikuwa nafasi, aliitengeneza mwenyewe na kuifanya kuwa nafasi, wakati mwingine hata wachezaji wetu wa Kitanzania wanapaswa kuiga mfano huu. Anaweza kuchukua mpira na akaamua sasa nifanye nini kwa manufaa ya timu, kusema kweli aina ya baadhi ya wachezaji waliokuwa nao Simba, akiwemo Sakho ndiyo ilioamua mechi si vinginevyo," alisema Juma.

Naye Matola alimpa sifa zake, lakini akaongeza Sakho pamoja na Banda uwezo wao umeonekana kuongezeka kwa sababu hawapi majukumu makubwa ndani ya uwanja, badala yake anawaacha wacheze huru.

"Ukiwapa majukumu mengine sijui wasirudi huku, mara wakabe, unawanyima uhuru wa 'kuinjoi' kucheza soka, mimi nimewapa uhuru wacheze mpira wanavyotaka wao, waende popote, wasiwe na kazi kubwa ya kukaba, ndiyo maana unaona viwango vyao halisi sasa," alisema Matola.

Sakho alifunga bao la kwanza, huku Banda akipiga krosi iliyomlazimisha kipa Shaaban Hassan 'Kado' kudakia ndani.



Wachezaji wa Azam FC ya Dar es Salaam wakifanya mazoezi ya mwisho kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya wenyeji Dodoma Jiji itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini humo. **PICHA: MTANDAO**

# Simba Queens kuibeba EOTF

**Na Saada Akida**

MCHEZO wa maalum wa kuadhimisha miaka 25 ya Taasisi ya Fursa Sawa kwa Wote (EOTF) inayoongozwa na mke wa Rais wa awamu ya tatu, Anna Mkapa kati ya Simba Queens dhidi ya Fountain Gate Princess utachezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo alisema jana mchezo huo ambao hakutakuwa na kiingilio utafanyika kuanzia saa 9:30 mchana na mgeni rasmi atakuwa ni Rais mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete.

"Kabla ya mchezo wa wanawake kutakuwa na mechi ya utangulizi kati ya wake wa viongozi dhidi ya wajasiriamali, hivyo tunawaomba mashabiki wa soka kufika kwa wingi," alisema Ndimbo.

Kuelekea mchezo huo makocha wa timu zote mbili akizungumzia mchezo huo walijinasibu kwa mchezo huo watatumia kwa ajili ya kuwatambulisha wachezaji wao wapya waliosajiliwa kwa ajili ya msimu ujao.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Nkoma alisema atatumia mechi hiyo kutambulisha baadhi ya wachezaji wake wapya waliosajiliwa msimu huu.

"Tumepata taarifa ya mechi timu tukiwa katika mapumziko, tunaenda kucheza kwa umuhimu mkubwa wa kupata ushindi lakini pia kutumia kwa ajili ya kutambulisha wachezaji wetu wapya," alisema Nkoma.

Naye Kocha Mkuu wa Fountain Gate, Juma Masoud alisema wamejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo huo ambao ni muhimu kwa pande zote mbili.

# Michezo

Jumamosi Juni 25, 2022
Nipashe



## Neymar alitaka taji la Ulaya akiwa PSG

# YANGA SC SHANGWE MBEYA, SIMBA IKIMNASA MPOLE

## Nabi afunguka wamedhamiria kuweka rekodi na heshima...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI mabingwa wapya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wanatarajiwa kuwakabili wenyeji Mbeya City katika mechi ya raundi ya 29 itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, Simba imefanikiwa kunasa saini ya straika wa Geita Gold FC, George Mpole.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi alisema mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu wenyeji wao wanakikosi imara, lakini wamejiandaa kupata matokeo mazuri.

Hata hivyo Nabi alisema wachezaji wake wanakabiliwa na uchovu kutokana na kucheza mechi mfululizo.

"Tunategemea mchezo utakuwa mgumu, lakini tumejiandaa na matokeo mazuri, tumecheza mechi mfululizo, kila baada ya siku mbili tunacheza, kwa hiyo kuna mchoko kwa wachezaji wangu, wanahitaji muda wa kupumzika pamoja na yote haya, lakini tuko makini," alisema Nabi.

Aliongeza mchezaji pekee ambaye ana uhakika atau-kosa mchezo huo ni Mkongomani Chiko Ushindi kutokana na majeraha.

Mbali na Yanga kuwa tayari imeshatwaa ubingwa wa msimu huu, lakini mechi hiyo itakuwa muhimu katika kuendeleza rekodi yake ya kutopoteza mechi hata moja.

Pia ni moja kati ya mechi ambazo zinaweza kumfanya straika wao, Fiston Mayele kupachika mabao katika harakati zake za kutaka kutwaa kiatu cha dhahabu huku wakibakiza mechi moja ambayo ni dhidi ya Mtibwa Sugar itakayochezwa Juni 29, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Viongozi na wadau mbalimbali wa Yanga, wako Mbeya kwa ajili ya sherehe hizo na baada ya hapo wanatarajiwa kusafiri kurejea Dar es Salaam na kupata mapokezi makubwa.

Taarifa za uhakika kutoka Simba zinasema tayari Mpole pamoja na winga wa Kagera Sugar, Nassoro Kapama wamesaini mkataba wa miaka miwili kila mmoja.

Nipashe liliwasiana na nyota hao, Mpole na Kapama ambapo walikiri kufuatwa na klabu kongwe hapa nchini na kuhakikisha kwamba baada ya msimu huu kufikia tamati wataweka wazi mipango yao.

"Ni kweli Simba na Yanga zilileta ofa zao ila ni wapi nitakwenda ni suala la muda ukifika litawekwa wazi kama ni Simba kama inavyotajwa tutajua baadaye," alisema Mpole.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally alisema ni kuhusu suala ya usajili kuna baadhi ya wachezaji wameshamalizana na kinachosubiriwa utambulisho.

"Usajili umekamilika kwa asilimi kubwa tumesajili vyuma vya hatari, kuhusu Okrah (Augustine), ni hatari anapiga mashuti balaa, mchakato wa kujiunga na Simba ni suala la muda," alisema Ahmed.

Aliongeza viongozi wa Simba wanafanya usajili kulingana na mahitaji ya kikosi chao na sio kwa sifa za kupiga picha na wachezaji ambao bado hawajasaini mkataba kwa ajili ya sifa.

"Tunafanya usajili kulingana na mapungufu yetu ya msimu huu, tunakubali tumepoteza lakini usajili tunaofanya msimu huu ni kabambe," Ahmed aliongeza.

Mshambuliaji wa Backem United ya Ghana, Okrah ni mmoja wa nyota wanaotajwa kuwindwa ndani ya kikosi cha Wekundu wa Msimbazi na kilichobakia ni muda kuzungumza.

Naye Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Selemani Matola akizungumzia mchezo wa juzi na Mtibwa Sugar alisema ulikuwa mgumu na amewapongeza wachezaji wake kufuata maelekezo na kufanikiwa kupata pointi tatu muhimu na kuwapa furaha mashabiki wao.

Kuelekea mechi dhidi ya Tanzania Prisons itakayochezwa kesho, Matola alisema watapambana kuhakikisha wanapata pointi zote sita kumaliza vizuri msimu kwa heshima.



Wachezaji wa Simba, Pape Sakho (kushoto) na Peter Banda wakifurahia bao katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Simba ilishinda mabao 2-0. **PICHA: SIMBA SC**

# Serengeti Girls, Ufaransa vitani

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya soka ya Taifa ya vijana ya wanawake wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), imepangwa katika Kundi D kwenye fainali za Kombe la Dunia (U-17), zitakazofanyika Oktoba mwaka huu nchini India.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa jana, Serengeti Girls iko kundi moja pamoja na Japan, Canada na Ufaransa wakati Kundi A linaundwa na wenyeji India, Marekani, Morocco na Brazil.

Ujerumani, Nigeria, Chile na New Zealand zinaunda Kundi B wakati Hispania, Colombia, Mexico na Jamhuri ya China wako Kundi C.

**Serengeti Girls iliyoko chini ya Kocha Mzalendo, Bakari Shime anayesaidiana na Edna Lema ilikata tiketi ya kushiriki fainali hizo kwa mara ya kwanza baada ya kuziondoa Botswana, Burundi na Cameroon.**

Kikosi hicho kinatarajia kuanza mazoezi kuelekea fainali hizo mapema mwezi ujao na kitasafiri kwenda nje ya Tanzania kuweka kambi ili kujiimarisha zaidi.

"Tunamikakati mizuri ya kuiandaa timu yetu kuelekea fainali hizi za Kombe la Dunia, TFF (Shirikisho la Soka Tanzania) kwa kushirikiana na serikali, tunaamini wachezaji wataimarika na kuwa tayari kwenda kupeperusha bendera ya nchi kwa heshima," Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo alisema.



Bakari Shime

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >